# DURU ZA UENDELEZAJI WA WRUA

## (WRUA DEVELOPMENT CYCLE) (WDC)

TOLEO LA PILI

APRILI 2014

## UTANGULIZI

Uamuzi wa kutafsiri toleo jipya la Nyaraka za WDC katika lugha ya Kiswahili, ulifikiwa kwa lengo la, kwa upande mmoja, kupanua usomaji na matumizi yao hasa katika ngazi za chini kupitia Jumuiya za Watumiaji wa Rasilimali Za Maji (Water Resources Users Associations WRUAs) ambapo ufahamu wa Lugha ya Kiingereza unaweza kuwa haba. Kwa upande mwingine tafsiri hii pia inalenga kutimiza matakwa ya kikatiba kwamba nyaraka za wananchi zinazohusiana na fedha za umma zitolewe katika lugha zote mbili: ya Kiingereza na ya Kiswahili.

Toleo jipya la WDC imeundwa kwa sehemu tatu zinazosaidiana ambazo zimewekwa pamoja katika sehemu tatu tofauti zinazogusia **Mfumo**, **Miongozo ya Uendeshwaji wa Shughuli**, na **Vifaa Vya Uendeshaji**. Mfumo unafafanua mipango ya kazi kati ya WRUAs, WRMA na WSTF kwa masuala ya Mafunzo na ufadhili wa usimamizi wa rasilimali za maji na utawala. Mfumo pia ukiwa na marekebisho kidogo unaweza kutumiwa na wadau wengine wa maendeleo wenye uwezo na nia ya kusaidia shughuli za WRUA katika nchi hii.


Tafsiri hii ya awamu ya kwanza, hata hivyo, haijashughulikia sehemu hizi tatu za WDC lakini inalenga Sehemu ya kwanza kuhusu Mfumo, na sehemu ya pili kuhusu Miongozo ya Uendeshwaji Shughuli, na kuacha nyongeza zinazohusika. Tulizipatia nafasi zaidi sehemu hizi mbili kwa sababu ziko na habari muhimu zaidi na zinalenga kutoa taarifa za utaratibu wa kuundwa kwa WRUA na utekelezwaji wake, ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa msaada wa fedha kutoka WSTF. Vifaa vya uendeshaji hutumika kutoa mafunzo kwa wanachama na jamii za WRUA kwa ujumla, juu ya vifungu vya Usimamizi wa Mkusanyiko wa Maji (Catchment Management Strategies CMS) kwa mujibu wa masuala ya Ufanisi wa rasilimali za maji wa mashinani. Katika wakati ujao, na iwapo uwezo utapatikana (WRMA na kiwango cha mashauri) kutumia vifaa vya mafunzo kwa Kiswahili, tunatarajia kutafsiri sehemu zilizobaki ili kuwa na toleo kamili la WDC kwa lugha ya Kiswahili.

Tunatambua na kuzishukuru taasisi na watu waliohusika katika utaratibu wa kutafsiri: hasa tunataka kutoa shukrani zetu kwa

*Wakala wa Uswisi kwa ajili ya Maendeleo na Ushirikiano* (Swiss Agency for Development and Cooperation SDC), kupitia *Taaasisi ya Mafunzo na Utafiti kwa Ustawi wa Maeneo Kame* (Centre for Training and Integrated Research in ASAL Development (CETRAD), kwa kufadhili tafsiri hii; timu kutoka taasisi hizi tatu ambazo zilitazama upya na kupangilia vifaa vya kutafsiriwa; na shirika lililotafsiri, na kuunda maandishi, *Mtaalamu Mshauri, Muandaaji Nakala kwa Kutumia Kompyuta - Mtandao wa Muundo wa Maandishi Africa, Nairobi* (Computer Aided Text Processing Technical Consultant - Africa Typesetting Network Ltd, Nairobi) kwa kazi nzuri waliyoifanya na kuikamilisha kwa muda uliofaa.

Sisi tunahimiza wafanyakazi wa WRMA, wanachama wote wa WRUA, washauri wanaotoa msaada kwa WRUA na kwa wananchi wote, wachukue nafasi ya toleo hili la Kiswahili na kulisoma ili kujifahamisha wenyewe na kuimarisha uelewaji wao kuhusu masharti ya WDC. Hii itasaidia sana kunyorosha malezi na uendeshwaji wa shughuli za WRUA, na hivyo kuboresha utendaji wao na ushawishi wao katika usimamizi wa rasilimali za maji katika maeneo yao wanapoendesha shughuli zao.

Tunawatakia nyote usomaji nzuri na uelewaji wa kina wa dhana ya WRUA.




Eng Phillip olum, HSC
*Mkurugenzi Mtendaji*
*WRMA*

Ismail F.M. Shaiye
*Mkurugenzi Mtendaji*
*WSTF*

Boniface Kiteme, PhD
*Mkurugenzi*
*CETRAD*

## WARAKA WA MAPITIO YA WDC KWA JUMLA

| Sehemu | Mada | Yaliyomo | Kumbukumbu | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| **1** | **MFUMO WA WDC** | WDC Utangulizi<br>Sera na mfumo wa utungaji wa sheria<br>WDC Mbinu za maelezo kwa jumla<br>WRUAs | | |
| | | | **Nyongeza** | |
| **2** | **MIONGOZO YA UENDESWHAJI WA SHUGHULI ZA WDC** | Maeneo na shughuli zilizoidhinishwa | **A1** | Mkataba wa Makubaliano wa WSTF – WRMA |
| | | Utaratibu wa Ufadhili wa WDC | | |
| | | Miongozo ya kifedha ya WDC | | |
| | | | | |
| | | | **A2** | WRMA-Washirika wengine wa Maendeleo – Mkataba wa Makubaliano |
| | | | **A3** | WRMA-WRUA Mkataba wa Makubaliano |
| | | | **B** | Kuorodheshwa mkusanyiko mdogo wa maji kulingana na hali |

| Sehemu | Mada | Yaliyomo | Kumbukumbu | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| | | | **C** | WDC Viwango wastani kwa WRUA |
| | | | **D1** | WDC Kuomba fedha (RFF) |
| | | | **D2** | WDC Kupeleka Fomu ya maombi ya fedha WRMA-WSTF |
| | | | **E** | Mpango wa usimamizi wa mkusanyiko mdogo wa maji (muhtasari) |
| | | | **F** | WDC Uchunguzi wa hapo kwa hapo |
| | | | **G** | WDC Uchunguzi wa mashinani |
| | | | **H** | WDC Shughuli za Mkataba |
| | | | **I** | WDC Ripoti ya Maendeleo (muhtasari) |
| | | | **J** | WRUA – SO mkataba (sampuli) |
| | | | **K** | Masharti ya WRUA kusajiliwa na WRMA |

| Sehemu | Mada | Yaliyomo | Kumbukumbu | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| | | | **L** | Mpango wa utekelezaji (Kutumia na Excel) |
| | | | **M** | WDC Chombo cha Ufuatiliaji wa Miradi (Viambatisho A- E) |
| | | | **N** | Muongozo wa Shughuli za Ufuatiliaji |
| | | | **Sehemu ya** | |
| **3** | **VIFAA VYA WDC** | Maelekezo ya vifaa kwa WDC | | |
| | | | **1** | Mageuzi ya Sekta ya Maji |
| | | | **2** | Maelezo ya jumla kuhusu WDC |
| | | | **3** | Sifa za mkusanyiko wa maji |
| | | | **4** | Kuimarishwa SCMP |
| | | | **5** | Maji ya ziada & Usimamizi wa Mahitaji ya Maji |
| | | | **6** | Mgao wa Maji na Matumizi ya Maji |
| | | | **7** | Ulinzi wa Maji Rasilimali |

| Sehemu | Mada | Yaliyomo | Kumbukumbu | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| | | | **8** | Uhifadhi wa mkusanyiko wa maji na Uhifadhi wa mito kwa wamiliki wa ardhi kando ya mito ya maji |
| | | | **9** | Usimamizi wa mafuriko |
| | | | **10** | Mabadiliko ya Hali ya Hewa |
| | | | **11** | Kuimarishwa Miundombinu |
| | | | **12** | Mapato mbadala ya kuishi |
| | | | **13** | Haki za Kimsingi na Njia za Kuondoa Umaskini |
| | | | **14** | Maendeleo ya Kitaasisi |
| | | | **15** | Ufuatiliaji na Habari |
| | | | **16** | Usimamizi wa Fedha |
| | | | **17** | Sehemu ya Mafunzo<br>Sehemu ya 2 Miongozo ya Uendeshwaji wa Shughuli |

# DURU ZA UENDELEZAJI WA WRUA

(WRUA DEVELOPMENT CYCLE WDC)

**TOLEO LA KWANZA**

**MFUMO**

## YALIYOMO

**DURU ZA UENDELEZAJI WA WRUA....................................... 1**

**UTANGULIZI ................................................................. 3**

**WARAKA WA MAPITIO YA WDC KWA JUMLA ............................. 5**

**1.1 UTANGULIZI ......................................................... 13**

1.1 Historia.................................................................13

1.2Mfumo wa Duru za Uendelezaji wa WRUA (WDC) ......................15

1.3Wadau Kushiriki katika Usimamizi wa Rasilimali za Maji ........15

*1.3.1 Usimamizi wa Rasilimali za Pamoja za Maji ..............................15*

*1.3.2 Kamati ya Ushauri ya Maeneo yenye Mkusanyiko wa Maji .........17*

*1.3.3 Jumuiya za Watumiaji wa Rasilimali Za Maji ..............................18*

1.4Sera na Mfumo wa Kisheria ...............................................20

*1.4.1 Katiba ya Kenya ya Mwaka wa 2010.......................................... 20*

*1.4.2 Karatasi ya Kikao No 1 ya mwaka 1999 kuhusu Sera ya Kitaifa ya Ufanisi wa Rasilimali za Maji na Maendeleo .............21*

*1.4.3 Sheria ya Mwaka 2002 Kuhusu Maji (Water Act 2002)...................22*

*1.4.4 Mkakati wa Ufanikishaji wa Rasilimali za Kitaifa za Maji ........... 23*

*1.4.5 Mkakati wa Usimamizi wa Mkusanyiko wa Maji ..........................24*

*1.4.6 Sheria za WRM ..................................................................24*

**2.MAELEZO YA MBINU ZA WDC ........................................ 26**

2.1Kanuni za kuelekeza ........................................................26

2.2Taswira ya Mfumo wa WDC ................................................28

**3.JUMUIYA ZA WATUMIAJI WA RASILIMALI ZA MAJI .............. 29**

3.1Utangulizi ...................................................................29

3.2WRUA ni nini? ..............................................................29

3.3Jukumu la WRUA katika Usimamizi wa Rasilimali za Maji........29

3.4Jukumu la jamii katika WRM...............................................30

3.5Malengo ya WRUA ..........................................................31

3.6Shughuli za WRUA Zilizoidhinishwa .....................................32

3.7Kusajiliwa WRUAs kama taasisi za kisheria ..........................32

3.8Kusajiliwa kwa WRUAs kwa WRMA.......................................33

3.9Nafasi na Maeneo ya Ardhi au Maji ya WRUA ........................34

3.10 Uanachama wa WRUAs ....................................................................34
3.11 Fedha za WRUA ..........................................................................36
3.12 Utaratibu wa Kubuniwa na kuundwa WRUA.............................37

**MIONGOZO YA UENDESHWAJI SHUGHULI WA WDC .................... 41**

## 1.1 UTANGULIZI

### 1.1 Historia

Ufanisi wa rasilimali za maji umekuwa hasa ukishughulikiwa na Katiba ya Kenya ya Mwaka wa 2010. Ibara ya 42 ya Katiba, huwezesha kila mtu haki ya mazingira safi na bora, ambayo ni pamoja na haki ya mazingira yaliyolindwa kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vizazi vijavyo. Maji safi na salama ni muhimu kwa mazingira haya bora. Ibara ya 43 inampa kila mtu haki ya maji safi na salama kwa wingi wa kutosha. Ufanisi wa Rasilimali za Maji ni muhimu kwa kuhakikisha utoshelevu huu. Katiba imetoa njia ya kuhakikisha hili kupitia Ibara 69 d na g.

Kabla ya kupitishwa kwa Katiba ya Kenya ya Mwaka wa 2010 sekta ya maji ilikuwa imefanyiwa mageuzi. Hii ilikuwa imeelezwa katika Karatasi ya Kikao No 1 ya mwaka 1999 kuhusu Sera ya Kitaifa ya Ufanisi wa Rasilimali za Maji na Maendeleo (Sessional Paper No. 1 of 1999 on National Policy on Water Resources Management and Development.) Sera hiyo iliwasilisha njia pana katika masuala ya jinsi rasilimali za maji zitasimamiwa na kuimarishwa nchini Kenya. Kutungwa kwa Sheria ya Mwaka 2002 Kuhusu Maji kulitoa mfumo wa kisheria kwa ajili ya usimamizi na maendeleo ya rasilimali za maji. Hili lilitaka kushughulikia matatizo yenye nafasi pana iliyokumbana na sekta hii ya maji hapo awali. Miongoni mwa masuala hayo ilikuwa ni haja ya kutenganisha utoaji huduma za maji kutokana na usimamizi wa rasilimali za maji kwa ajili ya utoaji wa huduma bora. Hii ilisababisha kuanzishwa kwa taasisi mbalimbali za sekta ya maji ikiwa ni pamoja na Wakfu wa Huduma za Maji (Water Services Trust Fund WSTF) na Mamlaka ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji (Water Resources Management Authority -WRMA).

WSTF ilianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Mwaka wa 2002 Kuhusu Maji (§83), ili kusaidia katika kufadhili huduma za maji katika maeneo yasiyonufaika ya Kenya. Katika utekelezaji wa mamlaka hayo, WSTF ilianzisha nafasi za ufadhili kwa ajili ya utoaji wa maji mashambani na mifumo ya maji mijini, ikilenga kimsingi maeneo ya vitongoji vya miji. Kwa kutambua kwamba zaidi ya 50% ya Wakenya hupata maji yao moja kwa moja kutokana na rasilimali

za maji (kuliko kupitia mfumo wa ugavi ulioboreshwa) na haja ya kulinda rasilimali za maji ambazo hutegemea utoaji wa maji, WSTF walifungua nafasi ya ufadhili ili kusaidia usimamizi wa rasilimali za maji mashinani, kupitia Jumuiya za Watumiaji wa Rasilimali Za Maji (Water Resources Users Associations WRUAs). Nafasi zilizopo kwa sasa za kufadhiliwa zinazopatikana kwa njia ya WSTF ni:

- Miradi ya Jamii za Mzunguko (Community Project Cycle CPC);
- Miradi isiyo ya Jamii za Mzunguko (Non-CPC);
- Dhana ya Miradi ya Mjini (Urban Project Concept UPC);
- Duru za Uendelezaji wa WRUA (WDC).

Mamlaka ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji (Water Resources Management Authority -WRMA) ilianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Mwaka wa 2002 Kuhusu Maji (§7) ili kusimamia, kufuatilia, kukagua na kutoa rasilimali za maji, kusimamia na kulinda mkusanyiko wa maji na kushirikiana na taasisi nyinginezo kama inavyotakiwa kwa ajili ya usimamizi bora wa rasilimali za maji. WRMA imepitisha Usimamizi wa Rasilimali za Pamoja za Maji (Integrated Water Resources Management IWRM) ambayo imesababisha matumizi yenye faida na maendeleo ya mkusanyiko wa maji na rasilimali za maji.

Wadau kushiriki katika usimamizi wa rasilimali katika ngazi ya mkusanyiko mdogo wa maji mashinani inaambatanishwa na kuibuka kwa Jumuiya za Watumiaji wa Rasilimali Za Maji (Water Resources Users Associations WRUAs). WRUAs ni jumuiya za uanachama wa hiari zinazoundwa na watumiaji wa maji na usimamizi bora wa wamiliki wa ardhi kando ya mito ya maji wenye nia ya usimamizi bora wa rasilimali zao za maji. WRUAs kwa muda zimesaidia kuelekeza ushiriki wa wadau unaohitajika katika njia ambayo husaidia kushughulikia baadhi ya matatizo sugu ambayo yamekuwa yakikabili usimamizi wa rasilimali za maji katika siku za nyuma. Kwa mfano, kiwango cha chini cha maarifa, matumizi duni ya ardhi na maji, viwango vya chini vya kufuata sheria na taratibu, ukosefu wa usimamizi mzuri, na kadhalika.

WRMA kwa kushirikiana na WSTF walianzisha mfumo wa WDC kupitishia uwekezaji katika usimamizi wa rasilimali za maji kwa ngazi za mashinani. Uwekezaji huu ni kwa madhumuni ya WRUA,

hasa katika maeneo ambapo rasilimali za maji zimejumulishwa katika hali ya "hatari" (yaani maeneo ya wasiwasi au maeneo ambayo hatua za dharura zinahitajika).

Kwa kuzingatia athari za mabadiliko ya hali ya hewa katika vyanzo vya maji ambayo imesababisha mafuriko, ukame na maporomoko ya ardhi, na asili ya WRUAs kuwa ya hiari, ni muhimu kwamba WRUAs zinaimarishwa kwa kitengo cha mapato ya kuishi kuingizwa katika shughuli zao ili kufikia usimamizi wenye ufanisi wa rasilimali za maji nchini Kenya.

## 1.2 Mfumo wa Duru za Uendelezaji wa WRUA (WDC)

Mfumo huu unafafanua mipango kati ya WRMA na WSTF kuhusu ufadhili wa shughuli za usimamizi wa rasilimali za maji kupitia WRUA. Hutoa miongozo ya kutosha kwa wadau wengine ambao wana nafasi za maendeleo wanaopendezwa na shughuli za WRUA. Inazidi kusisitiza haja ya ushiriki wa wadau na kushirikiana na WRUAs katika usimamizi wa rasilimali za maji.

## 1.3 Wadau Kushiriki katika Usimamizi wa Rasilimali za Maji

Katiba ya Kenya ya Mwaka wa 2010 Ibara 69 (d na g) inahifadhia nguvu Serikali wajibu wa kuhamasisha umma kushiriki katika usimamizi, ulinzi na uhifadhi wa mazingira. Serikali pia inawajibika kuondoa taratibu na shughuli ambazo zina uwezekano wa kuhatarisha mazingira. Sambamba na hilo, WRMA ikiwa ni chombo cha Serikali, inawajibika kuhakikisha ushiriki wa wadau katika usimamizi wa rasilimali za maji hivyo kutungwa kwa maandiko haya ili kuwezesha utoaji wa majukumu hayo yaliyotajwa hapo juu.

### *1.3.1 Usimamizi wa Rasilimali za Pamoja za Maji (Integrated Water Resources Management IWRM)*

Usimamizi wa Rasilimali za Pamoja za Maji (Integrated Water Resources Management IWRM) ni mfumo wa kimataifa wa kusimamia rasilimali za maji ambao huchukua mtazamo wa jumla wa rasilimali za maji kujumlisha kimazingira, kijamii na kiuchumi mazingira ya vyanzo vya maji. Upande mmoja katika sehemu mbalimbali za usimamizi wa rasilimali za maji ni kuhitaji

kusawazisha watumiaji mbalimbali na matumizi, na malengo kuambatanishwa yawe yanatazamwa kutoka kwa chanzo kimoja. Inatambulika kuwa watu tofauti wana malengo tofauti, mitazamo tofauti na maadili tofauti. Kupanga kwa manufaa ya kiuchumi kunahitaji kushughulikia gharama na faida zinazohusiana na chaguo fulani pamoja na uchambuzi wa nani ambao watagharamika na ni nani ambao watafaidika. Masuala ya ubora, uwajibikaji wa matukio; ubora wa mazingira na ustawi wa jamii ni muhimu kama vile ufanisi wa kiuchumi. Ni wazi kwamba haiwezekani kutunga lengo moja peke yake ambalo linatosheleza maslahi yote, wapinzani wote, na mtazamo wa kisiasa na wa kijamii (Loucks na wengine 1981). Kwa hiyo ni muhimu kwamba wadau wote kushauriwa na kushirikishwa katika usimamizi wa rasilimali za maji kwa njia ambayo maslahi yao / wasiwasi wao unaweza kuambatanishwa katika hatua za uongozi. Umuhimu wa kushiriki kwa wadau katika IWRM kulianzishwa katika Kongamano la Dublin (1992) na pia inahakikishwa kwa misingi ifuatayo:

- Watumiaji wa maji ambao wanashiriki katika uundaji na utekelezaji wa mpango wa usimamizi wa mkusanyiko mdogo wa maji wana uwezo zaidi wa kuelewa na kufuata;
- Watumiaji wa maji mashinani wenye maarifa ya asili au ya ndani ambayo ni muhimu kwa maendeleo na utekelezaji wa SCMP;

Ingawa kushiriki kwa wadau kumetambulika kuwa muhimu, kuanzisha utaratibu ambao wadau wanaweza kushiriki kikamilifu sio rahisi. Hii hasa ni kweli ambapo wadau wana asili tofauti za kijamii na kiuchumi, wametawanyika kwa maeneo makubwa, na wana vipaumbele tofauti sana na maono tofauti ya baadaye, na wana nia yenye faida katika vyanzo vya maji ambavyo vipo katika sehemu ngumu za mfumo wa maji. Kimsingi, haitoshi kudhani kuwa wadau wataweza kushiriki katika usimamizi wa rasilimali za maji. Hata hivyo, Katiba ya Kenya kwa mujibu wa Ibara 43 (d) inahitaji kwamba hatua za makini lazima zichukuliwe ili kusaidia makundi yaliyosahaulika kushiriki katika utaratibu wa usimamizi wa rasilimali za maji ili sauti zao zipate nafasi ya kusikizwa na mahitaji kushughulikiwa.

Sheria ya Mwaka 2002 Kuhusu Maji inahitaji wadau kushiriki katika maeneo yafuatayo:

- Uundaji wa Mkakati wa Ufanikishaji Rasilimali ya Kitaifa za Maji (National Water Resource Management Strategy NWRMS) {kifungu cha 11 (1)}
- Uundaji wa Mkakati wa Usimamizi wa Mkusanyiko wa Maji (Catchment Management Strategies CMS) {Sehemu 15 (1)}
- Utaratibu wa Kibali (Permits Process) (Sehemu ya 107)

Kuna taratibu mbalimbali kwa ajili ya mashauriano ya wadau. Hizi ni pamoja na ushiriki rasmi na taasisi zilizopo (kwa mfano: Kamati za Ushauri ya Maeneo yenye Mkusanyiko wa Maji (Catchment Area Advisory Committee CAAC)), taarifa kwa umma kupitia vyombo vya habari na matangazo ya umma katika mikutano ya mabaraza. Hata hivyo, mwingiliano na WRUAs wanaenda zaidi ya mashauriano tu ya umma, lakini unataka kuongeza ushiriki wa walengwa wa msingi (watumiaji wa maji).

### *1.3.2 Kamati ya Ushauri ya Maeneo yenye Mkusanyiko wa Maji (Catchment Area Advisory Committee CAAC)*

CAACs wanateuliwa na WRMA kwa kushauriana na Waziri wa Maji kwa mujibu wa kifungu cha 16 cha Sheria ya Mwaka wa 2002 Kuhusu Maji. Kamati hii inajumuisha wanachama wasiozidi idadi ya 15 kwa kila eneo lenye mkusanyiko wa Maji.

**a) Uanachama wa CAAC**

Kifungu cha 16 cha Sheria ya Mwaka wa 2002 Kuhusu Maji kinasema kwamba uanachama wa CAAC lazima kuwakilisha makundi yafuatayo ya wadau:

1. Mashirika ya Serikali
2. Mamlaka ya Maendeleo ya eneo
3. Jamii za Kulisha na Jamii za Kilimo;
4. Mashirika yasiyo ya Serikali
5. Wafanyabiashara
6. Serikali za Kaunti
7. Watu wanaojimudu

Ni vema kubainisha kwamba WRUAs hasa hazijatajwa kama moja ya makundi ya wadau ya kujumulishwa pamoja katika CAAC, ingawa Sehemu ya 16 (3) (f) imepeana kifungu cha sheria ambacho kinaweza kutumika kujumulisha WRM binafsi ambazo zaweza kukubalika kupokelewa kutoka kwa WRUAs kadhaa.

**b) Wajibu wa CAACs**

Sheria ya Mwaka wa 2002 Kuhusu Maji inasema kwamba jukumu la CAAC ni ushauri. Hii ina maana kwamba WRMA hailazimishwi na maamuzi ya CAAC, na kwamba mamlaka na wajibu wa maamuzi bado unabaki moja kwa moja na WRMA.

CAAC huchangia katika maeneo yafuatayo ya kimsingi:

(a) Rasilimali zinazohifadhi Maji, matumizi na mgawo;

(b) Utuoaji, Urekebishaji, kufutiliwa mbali au kubadilishwa kwa kibali chochote; na

(c) Masuala mengine yoyote yanayoambatana na usimamizi bora wa rasilimali za maji.

Ni vema kubainisha kwamba wanachama wa CAAC nia yao sio kuwa waakilishi wa watumiaji wa maji binafsi wa maeneo fulani bali waakilishi wa makundi ya wadau. Kimsingi hakuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya mtu binafsi mtumiaji wa maji na mwanachama wa CAAC.

### *1.3.3 Jumuiya za Watumiaji wa Rasilimali Za Maji (Water Resources Users Associations WRUAs)*

WRUA ni Jumuiya ya watumiaji wa maji, wamiliki wa ardhi kando ya mito ya maji, au wadau wengine ambao wamehusishwa rasmi na kwa hiari kwa madhumuni ya kushirikiana kugawana, kuendeleza na kuhifadhi rasilimali ya pamoja ya maji. (Hii ni kuambatana na kanuni za WRM).

Uamuzi wa kutumia ushiriki wa wadau kwa WRUA hupatikana kutoka kwa sehemu zifuatazo:

- Kanuni za Dublin 1992

- Historia thabiti ya kijamii na kiutamaduni katika uendelezaji wa pamoja wa rasilimali za asili na kanuni za kijamii zimeelezwa ndani ya mazingira ya jamii nchini Kenya
- Taratibu dhaifu za kisheria ambazo huleta "pengo tawala" ambapo maslahi ya pamoja hayawezi kutumika vizuri na hivyo muundo wa WRUA kulijaza pengo hilo;
- Hatua za kawaida na za pamoja za wadau zinaweza kutoa ushawishi mkali ambao unaweza kutumika kwa faida ya huduma za serikali, msaada na kushawishi mgao na matumizi ya rasilimali za maji kwa ajili ya maslahi ya pamoja;
- Ruwaza za mashinani za makazi, matumizi ya ardhi ya jamii (mfano maeneo yenye majimaji, misitu, malisho, na kadhalika) na tabia za matumizi ya maji yahitaji mbinu-msingi za jamii "kuanzia chini kwenda juu" kama maboresho yanayofaidi kwa rasilimali za maji yatanufaisha.

Jukumu la WRUAs limeimarishwa zaidi katika Kanuni za Usimamizi wa Rasilimali za Maji (Water Resources Management Rules). Mashuhuri miongoni mwa kanuni hizi ni zifuatazo:

- WRUA lazima kiwe chombo kilichosajiliwa kisheria ili kutambulika kama WRUA na WRMA. Hii ina maana kwamba WRUA lazima kutafuta usajili kisheria kutoka kwa Msajili wa Vyama vya Ushirika kama jumuiya;
- WRUA inayotambuliwa na WRMA itakuwa imeorodheshwa katika regista rasmi ya WRUA. Kuna kipengele rasmi kwa zoezi la WRUA kwa ajili ya chemchemi maalum ya maji au sehemu ya chemchemi maalum ya maji kuambatana na maeneo yanayoshugulikiwa na hiyo WRUA
- WRUAs wanaweza kuingia katika makubaliano rasmi ya mkataba (MOU) na WRMA kufafanua majukumu zaidi, wajibu na mipango ya kazi kwa ajili ya usimamizi wenye ushirikiano. Hii inatoa uwezekano mpana ambapo WRUA inaweza kuhusishwa katika shughuli kama vile kuchunguza rasilimali za maji na kushughulikia mawazo yanayotukia, na kadhalika. Iwapo WRUA inashindwa kuheshimu makubaliano hayo rasmi ya mkataba (MOU), basi itapigwa kalamu kutoka kwa regista ya WRMA. WRUA hii bado itakuwa imesajiliwa na Msajili wa Vyama lakini itakuwa haiwezi tena kuingiliana na WRMA hii;

## 1.4 Sera na Mfumo wa Kisheria

### *1.4.1 Katiba ya Kenya ya Mwaka wa 2010*

Katiba ya Kenya ya Mwaka wa 2010 imesambaza kazi za usimamizi wa rasilimali za maji kwa Serikali ya Taifa na kwa Serikali za Kaunti. Chini ya Ratiba ya Nne (Sehemu ya 1) Kazi za Usimamizi wa Rasilimali za Maji ambazo zimetengwa kwa Serikali ya Taifa zimekaririwa katika vipengee 2, 19, 22, 24, na 32. Hizi ni:

- Sec 2. Matumizi ya maji ya kimataifa na rasilimali za maji - ikimaanisha kudhibiti na kupimwa kwa matumizi ya maji kila mahali katika Jamhuri. Hii ni bila kujali chanzo cha maji kiko wapi.
- Sec 19. Ujenzi wa umma wa kitaifa - Rasilimali za Maji Maendeleo; hasa juu ya kuruhusu na kuhakikisha kufuata masharti ya ruhusa juu ya miundombinu ya kudumishwa kwa maji na ujenzi kwa chemchemi za maji
- Sec 22. Ulinzi wa mazingira na maliasili kwa lengo la kuunda mfumo wa maendeleo wa kudumu na wa kufaidi, ikiwa ni pamoja na, hasa:
- (c) Ulinzi wa maji, kupata maji ya kutosha yanayodumu, uhandisi wa maji (hydraulic engineering) na usalama wa mabwawa
- Sec 24. Kuthibiti maafa – Maafa yatokanayo na maji kama vile mafuriko, ukame na maporomoko ya ardhi
- Sec 32. Kukuza uwezo na misaada ya kiufundi kwa Kaunti

- Chini ya Ratiba ya Nne (Sehemu ya 2) Majukumu ya Kaunti yanayohusiana na Rasilimali za Usimamizi wa Maji yameelezwa katika Sehemu (10, 11 & 12) & 2.
- Sec 10. Utekelezaji wa sera maalum za serikali ya kitaifa juu ya maliasili na utunzaji wa mazingira, ikijumulisha pamoja na uhifadhi wa udongo na uhifadhi wa maji.
- Sec 11. Ujenzi wa umma katika kaunti na huduma, ikiwa ni pamoja na mifumo ya usimamizi wa maji ya dhoruba katika maeneo yaliyojengwa.
- Sec 12. Huduma za mazima moto na usimamizi wa maafa - hasa juu ya majanga yanayotokana na maji

- Sec 2. Huduma za Kaunti za Afya, ikiwa ni pamoja na hasa (g) kutoa maji taka, kutupa matakataka na kutupa takataka ngumu - ingawa hii si hasa kazi ya WRM; shughuli hizi zina athari kwa ubora wa maji na hivyo mipango yao inahitaji kutazamwa wakati wa mipango ya maeneo.
- Mipango na Maendeleo ya Kaunti, pamoja na (d) Kupima na kuchora ramani. Hii itakuwa ni muhimu sana katika jitihada zetu za kulinda maeneo ya ardhi ambayo yako kando ya mito, mito yenyewe, maziwa ya maji, chemichemi za maji, maeneo yenye majimaji na maeneo mengine nyeti kiikolojia kwa madhumuni ya kusimamia rasilimali maji.

Kazi zile zinazoshirikisha Serikali ya Taifa na Serikali za Kaunti zinazoomba ushirikiano kati ya serikali hizi mbili ni uhifadhi wa maji, usimamizi wa maji ya dhoruba na majanga yanayohusiana na maji; kwa mfano, usimamizi wa mafuriko. Mfumo wa WDC umeletea mafunzo ya WRUAs jinsi ya kutawala shughuli hizi katika SCMP. Serikali ya Taifa na Serikali za Kaunti hivyo kwa pamoja watashirikiana kutenda kazi ili kufikia malengo haya. Hii inaweza kuwa katika eneo la kuunganisha shughuli za SCMP katika Mipango Jumuishi ya Maendeleo ya Kaunti (County Integrated Development Plans CIDP), ikiwa ni pamoja na kufadhili.

### *1.4.2 Karatasi ya Kikao No 1 ya mwaka 1999 kuhusu Sera ya Kitaifa ya Ufanisi wa Rasilimali za Maji na Maendeleo (Sessional Paper No. 1 of 1999 on National Policy on Water Resources Management and Development.)*

Mfumo wa kusimamia na kuimarisha rasilimali za maji unategemea sana Karatasi ya Kikao No 1 ya mwaka 1999 (Sessional Paper No. 1 of 1999). Masharti muhimu katika sera ni:

1. Mgawanyo wa kazi (Usimamizi wa rasilimali za maji, utoaji wa huduma za maji, sera, sheria, kufadhili);
2. Kugawanya madaraka (Uhamisho wa kufanya maamuzi katika ngazi za Kitaifa na ngazi za mashinani / Kaunti);
3. Mambo ya biashara (Maji kutendewa kama mali ya kiuchumi na mali ya kijamii);
4. Wadau kushiriki kupitia jamii na sekta ya kibinafsi

### *1.4.3 Sheria ya Mwaka 2002 Kuhusu Maji (Water Act 2002)*

Mnamo Machi 2003 Sheria ya Mwaka 2002 Kuhusu Maji (Water Act 2002) ilianza kutumika. Sheria ya Mwaka 2002 Kuhusu Maji inatoa mfumo wa kisheria kwa kuzingatia mabadiliko mapya ya sera. Taasisi mpya zenye kazi tofauti ziliundwa, na kufanya maamuzi ya kugawanya madaraka na kusababisha kujitokeza kwa chemchemi huru za maeneo tofauti.

Taasisi zilizoundwa kwa mujibu wa Sheria ya Mwaka 2002 Kuhusu Maji kushughulikia usimamizi wa rasilimali za maji zinaonekana katika orodha ya maelezo hapa chini:

*Taasisi za Maji chini ya Sheria ya Mwaka 2002 Kuhusu Maji*

| Taasisi | | Wajibu na majukumu |
|---|---|---|
| 1. | Wizara inayosimamia masuala ya maji | •Ufanisi wa sheria, utungwaji wa sera, sekta ya uratibu na uongozi, na ufuatiliaji na ukaguzi. |
| 2. | Mamlaka ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji (Water Resources Management Authority -WRMA) | •Mipango, usimamizi, ulinzi na uhifadhi wa vyanzo vya maji.<br>•Mipango, mgao, ukaguzi na ufuatiliaji wa rasilimali za maji.<br>•Utoaji wa vibali vya maji.<br>•Kudhibiti haki za maji na masharti ya vibali.<br>•Kudhibiti miundo ya kuhifadhi maji na miundo ya uchotaji wa maji.<br>•Uongozi wa mkusanyiko wa maji na ubora wa maji.<br>•Kuweka kiwango cha maji na kudhibiti matumizi ya maji. |
| 3. | Kamati ya Ushauri wa Maeneo yenye Mkusanyiko wa Maji (CAAC) | •Kushauri WRMA juu ya usimamizi wa rasilimali za maji na ulinzi katika ngazi ya mkusanyiko wa maji. |

| Taasisi | | Wajibu na majukumu |
|---|---|---|
| 4. | Jumuiya za Watumiaji wa Rasilimali Za Maji (WRUAs) | •Ushirikishwaji katika utaratibu wa maamuzi kwa kutambua na kusajili watumiaji wa maji.<br>•Ushirikiano katika mgao wa maji na uongozi wa mkusanyiko wa maji.<br>•Kusaidia katika ufuatiliaji wa maji na ukusanyaji habari.<br>•Utatuzi wa migogoro na usimamizi wa mashirika ya rasilimali za maji |
| 5. | Wakfu wa Huduma za Maji (WSTF) | •Kufadhili shughuli za usimamizi wa rasilimali za maji katika maeneo madogo "hatari" ya mkusanyiko wa maji<br>•Kufadhili kwa maji na kwa usafi wa mazingira kwa utoaji wa vifaa na huduma kwa ajili ya utupaji salama wa maji taka (sanitation) kwa makundi yaliyosahaulika. |

### *1.4.4 Mkakati wa Ufanikishaji wa Rasilimali za Kitaifa za Maji (National Water Resource Management Strategy NWRMS)*

Sheria ya Mwaka wa 2002 Kuhusu Maji imeletwa kwa ajili ya maendeleo ya Mkakati wa Ufanikishaji wa Rasilimali ya Kitaifa za Maji (National Water Resource Management Strategy NWRMS) kuhusu jinsi rasilimali za maji zitakuwa zikisimamiwa, kulindwa, kutumika, kuimarishwa, kuhifadhiwa na kudhibitiwa. Juu ya upande wa WRUA na ufadhili, NWRMS hutoa mwito kwa ajili ya kuboresha ushiriki wa wadau (Sehemu ya 3) na hasa, majimbo Sehemu 5.7 inasema, "WRMAs zitafanya jitihada ya kusaidia WRUAs. Katika kufanya hivi nafasi itatolewa ili kuwawezesha kupata fedha zinazotolewa na WSTF na mashirika mengine yanayofadhili kwa ajili ya usimamizi na maendeleo katika maeneo yao wanayomiliki."

Zaidi ya hayo, NWRMS Sehemu 5.5.5 inasema kwamba makaratasi ya sera yatatungwa kwa kufafanua juu ya majukumu ya kitaasisi na majukumu ya kifedha kwa ajili ya maendeleo ya miundombinu ya rasilimali za maji.

Malengo makuu kwa upande wa vyanzo vya maji katika NWRMS ni:

- Kuhifadhi na kulinda maeneo ya mkusanyiko wa maji
- Kusimamia rasilimali za maji kwa ufanisi
- Kuongeza upatikanaji wa vyanzo vya maji (kupitia kukinga maji ya mafuriko na kuongeza ubora wa maji);
- Kuongeza matumizi ya maji kwa ajili ya kuboresha uchumi na kuboresha jamii;
- Kutunga taasisi zenye ufanisi na ambazo zimetega masikio vizuri;

### *1.4.5 Mkakati wa Usimamizi wa Mkusanyiko wa Maji (Catchment Management Strategies CMS)*

Sheria ya Mwaka 2002 Kuhusu Maji inahitaji kutungwa kwa Mkakati wa Usimamizi wa Mkusanyiko wa Maji (Catchment Management Strategies CMS) kwa kila eneo. Kwa kila eneo CMS imetungwa. CMS hizi zinaweka wazi kanuni, malengo, taratibu na mipangilio ya kitaasisi kwa ajili ya usimamizi, matumizi, maendeleo, uhifadhi na udhibiti wa rasilimali za maji katika kila mkusanyiko wa maji. Inatarajiwa kwamba CMS, kama inavyotakiwa chini ya Kifungu cha 15 (5 ) cha Sheria ya Mwaka 2002 Kuhusu Maji, utatoa ufafanuzi zaidi juu ya mipango ya kitaasisi kwa ajili ya ushiriki wa wadau, na hasa kwa ajili ya uundwaji na ushirikiano wa WRUA.

### *1.4.6 Sheria za WRM*

Wizara simamizi kwa masuala ya maji na WRMA, kwa kushirikiana na wadau wengine, hutayarisha seti ya kanuni zinazoambatana na Sheria ya Mwaka wa 2002 Kuhusu Maji ambazo awali zilichapishwa kwa gazeti la serikali la mwaka 2007. (Ilani ya Sheria 171 - Kanuni Simamizi za Rasilimali za Maji: Gazeti la Serikali ya Kenya Sehemu CIX nambari 64, 28 Septemba 2007, Nyongeza ya Sheria nambari 92). (Legal Notice 171 - The Water Resources Management Rules: The Kenya Gazette Vol. CIX No. 64, 28th September 2007, Legislative Supplement No. 92).

Sehemu ya 10 ya Sheria za WRM hasa inahusika na WRUAs na uhusiano kati ya WRMA na WRUAs. Masharti muhimu ni:

a. WRUAs wapate kibali kisheria kupitia Msajili wa Vyama kama Mashirika na wapate kutambuliwa rasmi kupitia kusajiliwa na WRMA;
b. WRUAs wanaweza kuingia makubaliano rasmi ya mkataba (MOU) na WRMA ambapo WRMA hiyo inaweza kutoa msaada wa kiutawala, kitaalamu na kifedha kwa WRUA hiyo;
c. WRUA ambayo itakiuka makubaliano hayo rasmi ya mkataba (MOU) inaweza kusimamishwa na / au kupigwa kalamu na WRMA

Katika kuboresha kwa mahusiano haya ya kazi, WRMA itatafuta maoni kutoka WRUA msingi kwa ajili ya maombi ya kibali cha maji (Sehemu ya 28).

# 2. MAELEZO YA MBINU ZA WDC

## 2.1 Kanuni za kuelekeza

Duru za Uendelezji wa WRUA (WDC) msingi wake uko katika kanuni mbalimbali muhimu. Hizi zimejadiliwa kwa kifupi hapa chini.

a. *Mikakati ya Usimamizi wa mkusanyiko wa maji (Catchment Management Strategies CMS) hutoa mikakati ya jumla wa usimamizi wa rasilimali za maji katika ngazi ya mkusanyiko wa maji*

CMS ni hati ambayo inaweka mbinu na vipaumbele kama ilivyokubaliwa kati ya wadau kuboresha upatikanaji wa rasilimali za maji katika eneo la mkusanyiko wa maji. Shughuli za mashinani lazima ziambatane na mbinu zilizowekwa katika CMS. CMS inatoa mfumo kwa njia ambayo wadau wote wanaweza kushirikiana kwa ajili ya usimamizi bora wa rasilimali za maji.

b. *Usimamizi wa mkusanyiko mdogo wa maji (Sub-Catchment Management Plan SCMP) ni mpango, uliotungwa na wadau (WRMA, WRUA na wengine) ambao unaweka mipango ya matukio ya kushughulikia matatizo yanayowakabili WRM hasa mkusanyiko mdogo wa maji*

Kila mkusanyiko mdogo wa maji huwa tofauti na unaweza kukabiliwa na matatizo mbalimbali na wadau wa mashinani wanaweza kuwa na vipaumbele tofauti. SCMP basi inakuwa mpango uliokubalika wa shughuli zinazolenga kutatua matatizo. SCMP inaweza kubadilika kama habari mpya inapatikana na matatizo kuibuka. Kama CMS, SCMP inatoa mfumo kwa njia ambayo wadau mbalimbali wanaweza kushirikiana kwa kuboresha rasilimali za maji katika mkusanyiko mdogo fulani wa maji.

c. *Umakini wa kuhusisha Wadau unatakiwa kupata ushiriki wao katika WRM*

Mbinu ya haki za kimsingi huona kwamba hatua za makini lazima zichukuliwe ili kusaidia makundi yaliyosahaulika ili yashiriki katika utaratibu wa usimamizi wa rasilimali za maji ili kwamba sauti zao ziweze kusikizwa na mahitaji yao kushughulikiwa. Kimsingi haitoshi kudhani ya kuwa wadau wote wataweza kueleza mahitaji yao katika usimamizi wa rasilimali za maji. Utaratibu wowote wa mashauriano

lazima kuchukua hatua kuhakikisha kuwa wadau wote wana nafasi ya kufahamishwa na kuelewa matokeo ya maamuzi yanayofanywa.

*d. WRUA kama chombo cha kushiriki kwa jamii katika Usimamizi wa Rasilimali za Maji*

WRUA hutoa chombo kinachofaa kote ambacho uhamasisha na kuratibu ushiriki wa watumiaji wa maji katika usimamizi wa rasilimali za maji. Uzoefu hadi sasa unaonyesha kuwa WRUA, kama itahamasishwa vema, itaweza kutoa mchango mkubwa zaidi, ambapo taasisi nyingine zitalazimika kujaribu kupambana ili kufikia upeo sawa na huu. Ushiriki wa WRUAs siyo tu kuhusu mashauriano, lakini ni kuhusu ushiriki halisi katika WRM.

Mabadiliko ya hali ya anga yana madhara makubwa kwa vyanzo vya maji ikiwa ni pamoja na mafuriko, ukame, maporomoko ya ardhi miongoni mwa mengine. Mfumo huu basi umeundwa ili kusaidia WRUAs kuimarisha na kutekeleza mipango ya mabadiliko ya hali ya hewa ili kukabiliana na changamoto hizi.

Kulinda na kuhifadhi mkusanyiko wa maji ni shughuli ambayo hutumia muda mwingi sana na inahitaji juhudi kubwa kutoka kwa wanachama wa WRUA na haina faida ya moja kwa moja kwa wanachama binafsi. Katika jitihada za kuboresha mapato yao ya kuishi, sehemu ya kuleta mapato kwa maisha yao imeingizwa katika mfumo wa WDC.

*e. Mfumo wa WDC unaheshimu mgawanyo wa majukumu kati ya WRMA na WSTF*

Jukumu la kawaida la WSTF ni kutenda kazi ya ufadhili, kuelekeza fedha za Serikali ya Kenya na fedha za wafadhili kwa maeneo yaliyolengwa, kwa baadhi ya aina za miradi, kwa maeneo ambayo yamechaguliwa kupitia kuorodhesha uzito wa mahitaji. WRMA ina jukumu la masuala ya kitaalamu ya miradi ili kuhakikisha kuwa miradi inatenda kazi kuelekea kuboresha upatikanaji wa rasilimali za maji.

## 2.2 Taswira ya Mfumo wa WDC

WDC ni utaratibu wenye uwazi wa kuchagua WRUAs na kufanya uwekezaji kupitia WRUAs kwenye WRM. Dhana ya jumla ni muhtasari wa hatua zifuatazo:

1. WRUA inaundwa na kusajiliwa. Utaratibu huu unaweza kuungwa mkono na WRMA na / au mashirika mengine;
2. Katika mkusanyiko mdogo wa maji ama chemchemi za maji katika maeneo "hatari" na maeneo "tahadhari" WRMA husaidia WRUA kuanzisha SCMP awali;
3. WRMA inaingia katika mkataba wa WDC na WRUA kuhusu msaada kwa ajili ya utekelezaji wa SCMP. Mkataba huu hupitishwa na WSTF.
4. Fedha hutoka moja kwa moja kwa WSTF kuenda kwa WRUA zikiwa na 15% ya ada ya usimamizi wa WRMA
5. WRUA inapata fedha, inazitumia hizo fedha katika shughuli na kutoa hesabu ya vile fedha zimetumika kwa kutoa Stakabadhi ya Uwajibikaji wa Matumishi ya fedha (Fund Accountability Statement) na taarifa za mapato;
6. WRUA inatuma maombi kwa ngazi inayofuata ya kufadhiliwa
7. Kila ombi kwa sehemu mpya ya fedha inaambatana na maelezo kuhusu shughuli za baadaye na mpango wa bajeti.

Mkataba WDC basi hutoa utaratibu "mviringo" unaowezesha WRUA kuomba fedha za ziada za shughuli mpya na kiasi cha bajeti kuambatana na masharti ya kupitishwa kwa ukaguzi wa matumishi ya fedha. Kama uwezo wa WRUA unaendelea kukua, basi kiwango cha juu cha bajeti kitaongezeka ili kuiwezesha WRUAs kushiriki katika miradi mikubwa na kushiriki katika miundombinu ya miradi ya maendeleo ambayo inahusiana moja kwa moja na kuhakikisha hifadhi na kuboresha kuegemea vyanzo vya maji.

## 3. JUMUIYA ZA WATUMIAJI WA RASILIMALI ZA MAJI (WATER RESOURCES USERS ASSOCIATIONS WRUAS)

Sehemu hii inaweka habari kwa jumla kuhusu kubuniwa, kuundwa na kufanikishwa kwa WRUAs.

### 3.1 Utangulizi

Nchini Kenya, taasisi za kijamii zinazojulikana kama Jumuiya za Watumiaji wa Rasilimali Za Maji (Water Resources Users Associations WRUAs) kwa sasa zinaundwa na kuimarishwa nchini kote. Uzoefu kutoka nchini kote unaonyesha kwamba WRUAs wanaweza kutenda kazi na kupiga hatua ya kutia moyo kuhusu usimamizi wa rasilimali za maji.

### 3.2 WRUA ni nini?

WRUA ni jumuiya ya watumiaji wa maji, wamiliki wa ardhi kando ya mito ya maji, au wadau wengine ambao wamekuwa kirasmi na kwa hiari yao wenyewe wakihusishwa kwa madhumuni ya kushirikishana kugawana, kusimamia na kuhifadhi rasilimali ya maji pamoja. Makala muhimu ya ufafanuzi huu ni:

- Uanachama wa WRUA ni wa hiari;
- WRUA ni shirika la uanachama, si shirika la huduma, na kwa hiyo lina uwezo kupitia ushiriki wa wanachama wake;
- Kukubalika kuwa mwanachama hutokana na uhusiano wa mtu binafsi kwa rasilimali ya pamoja ya maji, kama mtumiaji wa maji, au mmiliki ardhi kando ya mto wa maji au mmoja wa wadau;

### 3.3 Jukumu la WRUA katika Usimamizi wa Rasilimali za Maji

WRUA kama inavyotambuliwa katika Sheria ya Mwaka 2002 Kuhusu Maji huwakilisha mashirika ya kijamii ambayo huja pamoja kwenye vyanzo vya maji vilivyotajwa kwa ajili ya usimamizi wa vyama vya ushirika na utatuzi wa migogoro. Hii inaweza kuundwa karibu na rasilimali ya ziwa la maji, mtiririko maalumu wa maji ya ardhini, kijito cha maji au mto. Watumiaji wa maji ni pamoja na wakulima,

watumiaji wa maji manyumbani, watoa huduma za maji, watumiaji wa maji kibiashara, watumiaji wa maji viwandani, na kadhalika. Uanachama wa WRUA msingi wake ni makubaliano ya hiari baina ya wanachama wenyewe.

Jumuiya ya Watumiaji wa Rasilimali za Maji ni mfano wa kuigwa kwa jamii kushiriki katika usimamizi wa rasilimali za maji. Mfano huu umejengwa juu ya ushahidi ufuatao:

i. Kwamba watumiaji wa rasilimali ya maji, wakiwa wafaidikaji asili au wadau wa kwanza wa rasilimali za maji, wanapaswa kushirikishwa kimsingi katika usimamizi wa rasilimali za maji;
ii. Kwa kuwa mapato yao ya kuishi yanahusika, watumiaji wa rasilimali za maji wanaweza kuhamasishwa kushughulikia usimamizi wa rasilimali za maji ambazo zinafaidi maslahi yao muhimu na mazingira (kwa mfano ufuatiliaji juu ya shughuli haramu au kuhusu ukiukaji wa sheria, au matendo yanayohatarisha maisha, kupitishwa kwa matumizi bora ya ardhi, usimamizi wa shughuli za mkusanyiko wa maji, ukaguzi wa ndani wa habari za mashinani, na kadhalika);
iii. Kuna ufanisi zaidi (upande wa WRMA) kwa ajili ya WRUA kuhamasisha watumiaji wa maji ili kutatua matatizo katika ngazi za chini.

Kwa ujumla, kuanzishwa kwa WRUAs ni sehemu muhimu katika kuimarishwa kwa mpangilio wa kugawa maji (WAP), kama itakuwa ikitoa mfumo kwa njia ambayo WAP inaweza kutekelezwa kwa ufanisi na kutoa nafasi kwa ajili ya ushiriki wa jamii, ambayo ni muhimu kwa ajili ya kuimarisha WAP hiyo. Hata hivyo, ni lazima ieleweke kwamba ufanisi wa WRUA katika usimamizi wa rasilimali za maji ni sawia moja kwa moja na juhudi zinazowekwa katika WRUA na hii inategemea matatizo asili kwa rasilimali maalum ya maji.

## 3.4 Jukumu la jamii katika WRM

Vyanzo vya maji ni vigumu sana kudhibiti kwani huchukuliwa kama “mali ya umma” inayopaswa kupatikana kwa wote. Ulinzi

na usimamizi wa rasilimali hizi hurahisishwa kwa msaada na ushirikiano wa wadau wa jamii ya mashinani. Faida ya hizi ni:

(a) Maslahi tofauti, hasa yale ambayo ni madogo sana, yanawakilishwa katika utoaji wa maamuzi,
(b) Utekelezaji wa wale ambao hufanya maamuzi hutazamwa upya mara kwa mara na wale wanaoathirika na maamuzi hayo.

Hapo awali kazi za maendeleo zilichukuliwa na jamii kuwa kizuizi kwa kuboresha mabadiliko ya kijamii na jamii kuhepa ushirikiano wa pamoja. Mipango ya sasa hata hivyo imekuwa ushindi kwa jukumu la jamii kwani huleta mgawo wa madaraka, ushiriki wa maana, na uhifadhi wa maliasili. Kutia ushiriki wa jamii moyo huleta nafasi ya jamii kushiriki moja kwa moja katika maamuzi yanayowahusu na hivyo kufaidika na juhudi zao.

## 3.5 Malengo ya WRUA

Malengo ya WRUA yanaweza kujumulishwa pamoja na yafuatayo:

- Kukuza shughuli zilizodhibitiwa na sheria za matumizi ya maji;
- Kukuza mazoea bora ya usimamizi ili kufanikisha na kuimarisha matumizi ya rasilimali za maji;
- Kukuza mazoea ya uhifadhi wa maji ili kuhakikisha akiba ya kutosha ya maji ambayo inatimiza mahitaji ya mazingira, wanyamapori, mifugo na jamii zote zinazotegemea rasilimali za maji kwa kuteremkiwa na maji ya mto huo;
- Kujitahidi kupunguza migogoro katika matumizi ya rasilimali za maji na kushiriki kwa kutatua migogoro ile inayotokea;
- Kukuza hatua za kuhifadhi mkusanyiko wa maji ili kuimarisha kiasi cha maji na ubora wake.
- Kusaidia wanachama washiriki katika shughuli za uzalishaji mali (IGAs)
- Kujenga uwezo wa jamii kurekebisha athari za mabadiliko ya hali ya hewa
- Usimamizi kudhibiti kuingiza mafuriko katika shughuli za SCMP

### 3.6 Shughuli za WRUA Zilizoidhinishwa

Ili kutekeleza na kufikia malengo hayo yaliyo hapo juu, shughuli za WRUA zinaweza kuambatanishwa pamoja na yafuatayo:

a) Ubadilishanaji wa habari na mawazo kuhusu matumizi ya rasilimali za maji;
b) Ubadilishanaji wa habari na utekelezaji wa shughuli juu ya usimamizi wa mafuriko, mabadiliko ya hali ya hewa na ukabilianaji wa hali hiyo
c) Kujadili miradi iwezekanayo na matukio ambayo yanaweza kuathiri matumizi ya maji kwa lengo la kupata makubaliano ya wanachama wengine wa WRUA na umma;
d) Kutatua migogoro kuhusu matumizi ya maji;
e) Kufuatilia upatikanaji wa maji na matumizi yake;
f) Kushawishi kwa rasilimali za kuboresha upatikanaji wa maji, maji yaliyoaminika, maji yenye thamani au mambo mengine ya rasilimali za maji.
g) Kushawishi kwa rasilimali kwa ajili ya IGAs kuimarisha mapato ya kuishi

Ni muhimu kutambua kwamba baadhi ya shughuli zilizoorodheshwa ziko chini ya mamlaka ya WRMA. Kwa sababu hiyo, inapendekezwa kwamba WRUAs wazishughulikie kwa misingi ya ushirikiano na si kwa njia ya kusukumwa na WRMA. Hii itafanya WRUAs kuwajibika kwa wanachama wao kimsingi na sio kwa WRMA. Kama vile, WRUA lazima kuingia katika mkataba wa makubaliano (MOU) na WRMA kuhusu wajibu na majukumu yaliyokubalika kwa pande zote mbili.

### 3.7 Kusajiliwa WRUAs kama taasisi za kisheria

Ni sharti kwa WRUAs kuandikishwa chini ya Sheria ya Vyama vya Mashirika kama shirika. Hii inaleta mamlaka kisheria kwa WRUA kwani imeundwa kama chombo cha kisheria. Utaratibu huu unahusisha yafuatayo:

- Ada ya usajili kutoka ofisi ya Mkuu wa Sheria (Kwa sasa Shilingi 2,000.00 za Kenya)

- Kujazwa na kuhalalishwa kwa fomu kutoka Nyumba ya Sheria (Sheria House) kwa kutiwa saini na viongozi wa ofisi hiyo;
- Katiba iliyoandaliwa vizuri;
- Kumbukumbu za mikutano zinazoonyesha wazi uchaguzi wa viongozi wa ofisi;
- Regista ya wanachama waliojiandikisha
- Maelezo ya akaunti ya Benki

Usajili wa shirika huchukua muda wa miezi mitatu hadi miezi mitano, lakini wakati mwingine kuenda hadi muda wa zaidi ya mwaka mmoja. Hii ni kwa sababu kabla ya usajili itawabidi maafisa kuchunguzwa na Idara ya Kitaifa ya Ujasusi (National Security Intelligence Service NSIS) ili kuhakikisha kuwa shirika haina ajenda ya kisiasa au ajenda ya kupotosha.

### 3.8 Kusajiliwa kwa WRUAs kwa WRMA

Sheria za WRM za mwaka 2007 kifungu cha sheria namba 10 kinatoa idhini WRUA kukubaliwa na WRMA kama inatimiza masharti yafuatayo:
- Imesajiliwa kisheria kama shirika chini ya kitengo cha sheria kuhusu mashirika
- Ni lazima iwe na katiba ambayo inaambatana na usimamizi wa pamoja wa ushirikishi wa rasilimali za maji wa rasilimali ya pahali fulani na ambayo huendeleza ushiriki wa umma, ukabilianaji na migogoro, uingizaji wa masuala ya jinsia na mazingira yaliyoimarika.

WRUA ambao wamesajiliwa na WRMA wanaweza kuingia katika makubaliano ya mkataba (MOU) na WRMA ili kuelezea zaidi mipango ya pamoja ya kushirikisha, kwa kueleza wajibu na majukumu yao kikamilifu. Zaidi ya hayo, WRUA waliosajiliwa na WRMA wanaidhinishwa kupata msaada kwa WDC na wanajumuishwa pamoja katika utaratibu wa taarifa za umma za maombi ya kibali cha maji. WRUA ambao watapigwa kalamu na WRMA, kwa kushindwa kuambatana na makubaliano ya mkataba (MOU) watapoteza uhusiano wao na WRMA.

### 3.9 Nafasi na Maeneo ya Ardhi au Maji ya WRUA

Kwa rasilimali za maji ya mto, inapendekezwa kwamba WRUA itaundwa katika ngazi ya eneo la mkusanyiko mdogo wa maji. Kutokana na utata wa mfumo wa mkondo wa maji inatambulika kwamba hili ni eneo ambapo uongozi na mashauriano yanahitajika hasa kwa WRMA. Kutokana na hali hii, WRMA wametenga mkusanyiko mdogo wa maji kwa mujibu wa mkondo wa maji kufuata mfano wa nchi nzima. Ramani ya kuonyesha WRUAs zilizopo na uwezekano wa zile zitakazokuja imetengenezwa na inapatikana katika ofisi zote WRMA.

### 3.10 Uanachama wa WRUAs

Uanachama wa shirika unasimamiwa na katiba ya wanachama wenyewe. Tukiomba kutokana na uzoefu wa WRUAs zinazotenda kazi nchini inapendekezwa kwamba uanachama wa WRUA sharti uundwe ukijumulisha makundi yafuatayo, yaani:

i. Wanachama wamiliki wa ardhi kando ya mito ya maji;
ii. Wanachama ambao huchota maji (Abstractor Members);
iii. Wanachama wasiotumia maji;
iv. Wanachama watazamaji.
v. Vikundi vya kijamii (CBOs) na Vikundi vinavyojitegemea (SHGs)

***(A) Mwanachama mmiliki wa ardhi kando ya mto wa maji***

Mmiliki wa ardhi kando ya mto wa maji (yaani ardhi inayoshikana na mto wa maji) ana haki ya uanachama wa Shirika kama Mwanachama Mmiliki wa ardhi kando ya mto, hata kama mwanachama hachoti maji moja kwa moja kutoka kwa chemchemi ya maji. Mmiliki wa ardhi kando ya mto wa maji ana haki ya uanachama mmoja peke yake, bila kujali ukubwa au idadi ya viwanja anavyomiliki. Uanachama wa mmiliki wa ardhi kando ya mto wa maji haimpatii kwa vyovyote vile mwanachama huyu idhini ya kuchota maji bila kibali.

*(B) Mwanachama anayechota maji (Abstractor)*

Mwanachama anayechota maji ni mtu, mpango, mradi ambao unachota maji kutoka kwa chemchemi ya maji na ambao unapaswa kuwa na kibali cha uchotaji huo. Aina hii ya mwanachama inaweza kugawanywa zaidi kuonyesha aina tofauti za uchotaji huu wa maji, na ni pamoja na:

i. Miradi ya maji au mipango – kimsingi kwa ajili ya matumizi ya nyumbani lakini yakihudumia familia nyingi;
ii. Watu binafsi - kimsingi kwa ajili ya maji ya nyumbani;
iii. Uchotaji kwa ajili ya matumishi ya umwagiliaji maji;
iv. Uchotaji kwa ajili ya matumishi ya viwandani - kimsingi kwa ajili ya viwanda;
v. Matumishi kwa ajili uzalishaji wa Mifugo;
vi. Uchotaji kwa ajili ya matumishi ya aina nyengine ya kibiashara;

*(C) Mwanachama asiyetumia maji*

Mwanachama asiyetumia maji ni mtu, biashara au chombo kingine kilichosajiliwa kisheria, ambaye anatumia chemchemi ya maji kama sehemu ya biashara yake au mapato yake ya kuishi, lakini ambaye hachoti kutoka kwa chemchemi ya maji. Vyama vya ushirika vya uvuvi vya kutumia jenereta za umeme wa maji hutumika kama mifano.

*(D) Mwanachama Mtazamaji*

Mwanachama Mtazamaji ni sehemu ambayo haipigi kura. Uanachama huu unakuwa wazi kwa mtu binafsi, shirika, au serikali ambao wanataka kushiriki katika shughuli za Shirika. Washauri wa kitaalamu na / au maofisa wa serikali ambao wameombwa na Shirika kutumikia kwa maslahi ya Shirika watajumulishwa kama Mwanachama Mtazamaji.

*(E) Vikundi vya kijamii (CBOs) na Vikundi vinayojitegemea (SHGs)*

Hivi ni vikundi vya kusajiliwa na Huduma za Jamii katika ngazi za Serikali za Kaunti na kushiriki katika shughuli maliasili msingi kuambatana na mkusanyiko mdogo wa maji. Makundi haya lazima kusajiliwa na WRUAs na sharti yaambatanishwe na makundi yaliyofadhiliwa na WRUA. CBO ina haki ya uanachama mmoja tu.

## 3.11 Fedha za WRUA

Mashirika mengi yanahitaji fedha ili kutenda kazi na kufanya shughuli zao, na WRUAs hazijatolewa kwa orodha hii. Zaidi ya hayo, WRUAs, kama vile mashirika mengine, zinahitaji kuimarisha mifumo kabambe ya fedha ambayo hujumuisha akaunti ya benki, regista ya mali zao, bajeti zao na stakabadhi kuonyesha jinsi matumizi ya fedha yalivyo, ukaguzi, mifumo ya ununuzi na taarifa za matumishi ya fedha kwa wanachama.

Kwa upande wa kutafuta fedha, nafasi mbalimbali zipo wazi za kuchaguliwa na WRUAs, ambazo ni pamoja na:

i. Kindani: malipo ya usajili wa uanachama na kujisajili upya kila mwaka, michango ya hiari, malipo kwa ajili ya huduma zinazotolewa na WRUA;
ii. Mamlaka ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji (Water Resources Management Authority -WRMA) inaweza kusaidia WRUAs moja kwa moja au kwa njia nyingine ikitegemea mahitaji, hali ya umuhimu wa shughuli iliyolengwa, na kujiamini kwa WRUA kuweza kutekeleza shughuli hiyo. Shughuli hizi zinaweza kujumlishwa pamoja na shughuli za kukuza uwezo, warsha za kupanga, mgawanyo wa wamiliki wa ardhi kando ya mito ya maji, kulinda mkusanyiko wa maji, ukusanywaji wa takwimu za rasilimali za maji, utungaji wa miundo na utungaji wa mapendekezo ya kufadhiliwa kwa ajili ya miundombinu ya rasilimali kubwa za maji (mabwawa, ulinzi mafuriko, na kadhalika).
iii. Wakfu wa Huduma za Maji (Water Services Trust Fund WSTF): WSTF watasaidia kufadhiliwa kwa mapendekezo ya kufadhiliwa yaliyowasilishwa na WRUA na kukaguliwa na WRMA. Fedha hizi zitaelekezwa:

⇒ Uanzishwaji na utekelezaji wa mipango ya usimamizi wa mkusanyiko mdogo wa maji;
⇒ Kujenga ufuataji wa kanuni (mita kuu za maji, ukarabati wa utumiaji, na kadhalika)
⇒ Uanzishwaji wa kuhifadhiwa kwa maji, kuanzia uhifadhi wa kiasi kidogo cha maji hadi uhifadhi wa kiasi kikubwa cha maji au kukingwa kwa mafuriko ya maji;
⇒ Uhifadhi wa mkusanyiko wa maji na ulinzi kando ya mito.
⇒ Mafunzo na kukuza uwezo kwa wanachama na wadau wa WRUA
⇒ Uhamasishaji wa watumiaji wa rasilimali za maji katika shughuli za WRM
⇒ Shughuli zinazohusiana na ukabilianaji wa migogoro ya matumizi ya maji
⇒ Uundaji na utekelezaji wa mipango ya mgao wa maji
⇒ Ujenzi uambatanao na uzuiaji wa maporomoko na uzuiaji wa mmomonyoko wa ardhi
⇒ Ujenzi uambatanao na ulinzi, uhifadhi au uimarishwaji wa ubora wa rasilimali za maji.

iv. Hazina ya Ufadhili wa Maendeleo ya maeneo jumbe (Constituency Development Fund CDF) kupitia kamati ya CDF
v. Hazina ya Ustawi wa Jamii (Community Development Trust Fund CDTF) - wana mipango miwili; mpango wa maendeleo ya jamii; na mpango wa Kuiwezesha Jamii kuhifadhi mazingira, zote mbili zikiwa na sehemu ya maji na sehemu ya usafi wa mazingira kwa utoaji wa vifaa na huduma kwa ajili ya utupaji salama wa maji taka (sanitation). WRUAs wanaweza kutuma maombi ya kufadhiliwa kwa CDTF kwa kutumia fomu za maombi zilizopendekezwa.
vi. Serikali za Kaunti
vii. Kuandika mapendekezo ya kufadhiliwa kwa wafadhili wengine wenye nia katika usimamizi wa maliasili


## 3.12 Utaratibu wa Kubuniwa na kuundwa WRUA

Utaratibu wa kubuniwa na kuanzishwa WRUA hufuata hatua tatu pana. Kila hatua ina sifa fulani kama inavyoonyeshwa wazi hapa chini:

| Hatua ya Maendeleo ya WRUA | Vipengele vinavyoeleza | Viashiria |
|---|---|---|
| **Hatua ya kubuniwa** | Uanachama unaelezeka kihafifu | Orodha ya wanachama haijaimarishwa bado |
| | Mipango ya usimamizi ni ya mpito | Kamati ya usimamizi wa uanachama ni wa mpito |
| | Mifumo ya kifedha ni midhaifu, hakuna uhakika wa kupata fedha za kutosha | Hakuna akaunti ya benki, hakuna rekodi vile fedha zinavyotumika |
| | Usajili unaendelea | Hakuna usajili |
| | Katiba inaendelea kutungwa | Hakuna katiba |
| **Hatua ya kulelewa** | Usajili rasmi unathibitishwa | Usajili unafika kwa ofisi ya msajili / Cheti cha usajili kinapatikana |
| | Mifumo ya usimamizi ni mpya na ni ya muda | Usimamizi usio na uhakika |
| | Mifumo ya utawala ni mpya na bado haijapimwa | Mwamko mdogo wa masharti katika katiba, uzingatiaji wa chini wa katiba |
| | Vigezo vya kuwa mwanachama havijaeleweka kwa wingi, namba ya uanachama inaongezeka | Rekodi za uanachama |
| | Mifumo ya kifedha inaendelea kuwa bora | Kitabu cha uendeshwaji wa shughuli<br>Kitabu cha mipango ya fedha<br>Kitabu cha shughuli za ununuzi kinaanza kutengenezwa |
| | Migogoro ya rasilimali inatambuliwa | Migogoro ya rasilimali inaendelea bila maazimio yanayoonekana wazi |

| Hatua ya Maendeleo ya WRUA | Vipengele vinavyoeleza | Viashiria |
|---|---|---|
| | Mipango ya kutenda mambo ni ya muda mfupi na ya upeo ambao haujapanuka | Mipango ya kutenda mambo imetekelezwa kwa uchache |
| **Hatua ya kukomaa** | Miundo ya utawala inaendeshwa na imefanyiwa majaribio | Mikutano ya kila mwaka (AGM), uchaguzi, ubora wa uongozi, zote zinazingatia katiba |
| | Mifumo ya kifedha imeundwa vizuri, kuna uwajibikaji na uwazi | Rekodi za kifedha zilizokaguliwa |
| | Uanachama u wazi, unatenda kazi, na uko imara | Rekodi za uanachama<br>Mwamko wa uanachama wa shughuli za WRUA (mfumo wa mawasiliano unatenda kazi) |
| | Usimamizi ni wa kitaalamu, ufanisi, na unaendeshwa kwa njia ya jinsi kazi inavyotendwa | Kumbukumbu za usimamizi, utekelezaji na mipango ya kutenda |
| | Mfumo upo na unapewa nafasi katika kushughulikia migogoro ya rasilimali | Migogoro ya rasilimali inatambuliwa na hatua zinachukuliwa |
| | Mipango ya kutenda imetungwa kuenea nafasi pana na kiwango kipana | Mipango ya hatua kutekelezwa |

Utaratibu wa kubuniwa na kuundwa WRUA pia umeelezwa kama seti ya hatua kama zilizopangwa, kama inavyoonekana katika Kielelezo 1, ambapo kiwango cha ufahamu wa kijamii na ushiriki huongezeka kwa kila hatua inayopigwa.




**Kielelezo 1: Utaratibu wa kubuniwa na kuundwa WRUA - Hatua Muhimu**

## SEHEMU YA PILI

# MIONGOZO YA UENDESHWAJI WA SHUGHULI ZA WDC

## (WDC OPERATIONAL GUIDELINES)

## TOLEO LA PILI

Umetungwa na

Halmashauri ya
Usimamizi wa Rasilimali za Maji

&

Wakfu wa Huduma za Maji

## YALIYOMO

**MIONGOZO YA UENDESHWAJI SHUGHULI WA WDC .................... 41**

**NYONGEZA ........................................................................... 45**

**1. DURU ZA UENDELEZAJI WA WRUA (WDC) ................................ 47**

1.1WSTF-WRMA Mkataba wa Makubaliano ......................................47

1.2WRMA – washirika wengine wa maendeleo Mkataba wa Makubaliano ..........................................................................47

**2.MAENEO NA SHUGHULI ZILIZOIDHINISHWA ........................... 48**

2.1 Viwango vya mkusanyiko wa maji..............................................48

2.2 WRUAs Changa.........................................................................53

2.3 WRUAs waliokomaa..................................................................53

2.4 Shughuli zilizoidhinishwa..........................................................54

**3 UTARATIBU WA UFADHILI WA WDC ........................................ 57**

3.1 Utangulizi ..................................................................................57

3.2 WRUA Kustahili Msaada wa Kifedha ..........................................58

3.3 Fomu za maombi / Maombi kwa ajili ya kufadhiliwa ................59

3.4 Mpango wa Usimamizi wa Chemichemi ndogo za Maji (Sub-Catchment Management Plan SCMP)...................................59

3.5 Utaratibu wa Kukaguliwa Maombi ..............................................59

*3.5.1 Ukaguzi wa hapo kwa hapo*..................................................59

*3.5.2 Ukaguaji wa mashinani*........................................................ 60

*3.5.3 Shughuli za Makubaliano ya WDC* ....................................... 60

3.6 Utekelezaji wa Usimamizi wa Chemichemi ndogo za maji (Sub-Catchment Management Plan SCMP) ......................60

3.7 Ufuatiliaji wa Mamlaka ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji ..........................................................................................61

3.8 Ripoti ya Shughuli za Maendeleo ...............................................61

**4.MWONGOZO WA WDC WA KUFADHILI...................................... 62**

4.1 Mipaka ya Uwekezaji ..................................................................62

4.2 Mchango kutoka Mashinani ........................................................62

## NYONGEZA

| | |
|---|---|
| Nyongeza A1- | Mkataba wa Makubaliano wa WSTF – WRMA |
| Nyongeza A2- | WRMA-Washirika wengine wa Maendeleo – Mkataba wa Makubaliano |
| Nyongeza A3- | WRMA-WRUA Mkataba wa Makubaliano |
| Nyongeza B- | Kuorodheshwa mkusanyiko mdogo wa maji kulingana na hali |
| Nyongeza C- | WDC Viwango wastani kwa WRUA |
| Nyongeza D1- | WDC Kuomba fedha (RFF) |
| Nyongeza D2- | WDC Kupeleka Fomu ya maombi ya fedha WRMA-WSTF |
| Nyongeza E- | Mpango wa usimamizi wa mkusanyiko mdogo wa maji (muhtasari) |
| Nyongeza F- | WDC Uchunguzi wa hapo kwa hapo |
| Nyongeza G- | WDC Uchunguzi wa mashinani |
| Nyongeza H- | WDC Shughuli za Mkataba |
| Nyongeza I- | WDC Ripoti ya Maendeleo (muhtasari) |
| Nyongeza J- | WRUA – SO mkataba (sampuli) |
| Nyongeza K- | Masharti ya WRUA kusajiliwa na WRMA |
| Nyongeza L- | Mpango wa utekelezaji (Kutumia na Excel) |
| Nyongeza M- | WDC Chombo cha Ufuatiliaji wa Miradi (Viambatisho A- E) |
| Nyongeza N- | Muongozo wa Shughuli za Ufuatiliaji |

# 1. DURU ZA UENDELEZAJI WA WRUA (WDC)

WDC ni mfumo ambao juu yake WRMA / WSTF / wadau wengine wa maendeleo watapatia fedha / msaada wa kitaalamu WRUAs ambazo zimeidhinishwa kutekeleza Usimamizi wa mkusanyiko mdogo wa maji (Sub-Catchment Management Plan SCMP) ili kuboresha mkusanyiko wa maji na rasilimali za maji.

Malengo ya miongozo ya WDC ni:

- Kuboresha wingi na ubora wa rasilimali za maji na kuongeza mapato ya kuishi;
- Kuboresha uwezo wa mkusanyiko wa maji na maeneo ya mito ya maji ili kutoa huduma za nishati ya maji;
- Kuboresha utawala wa rasilimali za maji kwa kukuza ushiriki wa wadau katika WRM;
- Kuboresha kufuata kanuni za maji na mazingira;
- Kujenga ujasiri wa jamii kwa mabadiliko ya hali ya hewa, na kukabiliana na hali hiyo
- Kuimarisha uwezo wa WRUAs kudhibiti mafuriko kwa ufanisi
- Kujenga WRUAs zinazotawaliwa vizuri na zinazojitegemea.
- Kukuza shughuli mbadala za mapato ya kuishi kwa kutoa misaada midogo midogo kwa ajili ya kufanikisha WRUA

## 1.1 WSTF-WRMA Mkataba wa Makubaliano

Mkataba wa Makubaliano (Memorandum of Agreement MOA) wa WSTF-WRMA ambao ni nguzo ya WDC unaonyeshwa katika Kiambatisho A.

## 1.2 WRMA – washirika wengine wa maendeleo Mkataba wa Makubaliano

WRMA-Washirika wengine wa Maendeleo – Mkataba wa Makubaliano (Memorandum of Agreement MOA) ambao ni nguzo ya WDC unaonyeshwa katika Kiambatisho B

## 2. MAENEO NA SHUGHULI ZILIZOIDHINISHWA

### 2.1 Viwango vya mkusanyiko wa maji

WDC nia yake ni kuelekeza fedha kwenye maeneo ambapo yana mahitaji makubwa zaidi. WRMA imeanzisha utaratibu wa kuweka kiwango kilichokubalika, ambacho kiwango cha chemichemi ya maji kinatambuliwa kwa kulingana na umuhimu wa kutenda kama inavyoonekana katika Jedwali 1.

*Jedwali 1: Kugawa mkusanyiko wa maji Kulingana na umuhimu wa hatua itakayochukuliwa*

| Kiwango | Hali ya rasilimali | Inavyomaanisha |
|---|---|---|
| **Kiwango 1** | **MAENEO HATARINI** | |
| Maji juu ya uso wa dunia | Mara kwa mara Rasilimali ni haba<br>Hifadhi za maji kutishwa | Mita za maji, kufuatilia na kudhibiti uchotaji wa maji<br>Hali ya kuhifadhi maji kwa siku tisini kunahitajika |
| Maji chini ya uso wa dunia | Kushuka kwa kiwango cha maji | Kubaini na kuweka kwa Gazeti rasmi la Serikali eneo la hifadhi ya maji<br>Mita za maji, kufuatilia na kudhibiti uchotaji wa maji |
| Ubora wa maji | Mkusanyiko wa maji kupunguza maji sana<br>Uchafuzi wa mazingira kwa kiwango cha juu<br>Hatari kwa maisha ya binadamu iko kwa kiwango cha juu | Kufuatilia na kudhibiti uchafuzi kutokana na maji taka (chanzo cha uchafuzi wa maji taka)<br>Kuanzisha na kushawishi kupunguzwa kwa uchafuzi wowote usiotokana na chanzo cha maji taka |
| Migogoro | Uwezekano wa migogoro u kwa kiwango cha juu | WRUAs lazima zikuzwe kikamilifu |

| Kiwango | Hali ya rasilimali | Inavyomaanisha |
|---|---|---|
| **Kiwango 2** | **MAENEO YA TAHADHARI** | |
| Maji juu ya uso wa dunia | Mwenendo unaelekea uhaba wa maji | Kufuatilia na kupanga hatua ya kutenda |
| Maji chini ya uso wa dunia | Mwenendo unaelekea uchotaji mwingi wa maji | Kufuatilia na kupanga hatua ya kutenda |
| Ubora wa maji | Mwenendo unaelekea upungufu wa ubora wa maji | Kufuatilia na kupanga hatua ya kutenda |
| Migogoro | Viungo vinavyosababisha migogoro, kwa mfano ukabila, kidini, mgawanyiko wa lugha tofauti | WRUAs zianzishwe |
| **Kiwango 3** | **MAENEO YANAYORIDHISHA** | |
| Maji juu ya uso wa dunia | Rasilimali za maji za kutosha kwa wingi na ubora wa maji | Uwezo wa kuhifadhi maji kwa muda wa siku tisini<br>Mita zinahitajika |
| Maji chini ya uso wa dunia | Hakuna madhara yanayodhibitika | Mita zinahitajika |
| Ubora wa maji | Ubora wa maji wa kutosha, kiwango kidogo cha hatari | Vibali vya uchafuzi kutokana na maji taka zinahitajika |
| Migogoro | Kiwango kidogo cha kutukia hatari ya migogoro | WRUA zinahitajika |

*(Kutoka: MWI 2007 Uendeshwaji Shughuli za Sheria ya Maji upande wa Usimamizi wa Rasilimali za Maji)*

*(Source: MWI 2007 Operationalization of Water Act with respect to Water Resources Management)*

Mkusanyiko mdogo wa maji unaowekwa katika hali ya hatari pia unaweza kuelezwa kuwa katika hali ambayo “hatari inaweza ikatokea wakati wowote” ambapo hatua za dharura zitahitajika mara moja. Dhana ya mkusanyiko mdogo wa maji ni ule ambao uko katika hali ya hatari , au mkusanyiko mdogo wa maji ambao “hatari inaweza kutokea wakati wowote” ni pale ambapo kuna hatari hapo kwa hapo ya hifadhi ya maji, utoaji wa maji, mipango ya usambazaji wa maji (kwa mfano nguvu za umeme) au hatari ya migogoro.

Kwa sasa kuorodheshwa kwa chemichemi za maji kulingana na hali kumefanywa kwa njia ya maoni ya kimsingi, kwa kuzingatia uzoefu wa wafanyakazi wataalamu wa WRMA na matukio ya matatizo katika ngazi ya rasilimali. Katika siku zijazo inatarajiwa kwamba kuorodheshwa kutafanywa kwa mbinu kali zaidi na kuthibitisha hadhi za chemichemi za maji kuambatana na malengo ya ubora wa rasilimali.

Jedwali iliyo hapa chini ni ziada ya jedwali 1 ambayo iko hapo juu ili kuingiza shughuli za mapato ya kuishi, kukabiliana na hali ya mabadiliko ya hewa, usimamizi wa mafuriko na ushirikiano wa WRM katika ngazi Kaunti.

*Jedwali 2: kugawa maeneo ya mkusanyiko wa maji kulingana na umuhimu wa hatua itakayochukuliwa*

| Kiwango | Hali ya rasilimali | Inavyomaanisha |
|---|---|---|
| **Kiwango 1** | **MAENEO HATARINI** | |
| Maji juu ya uso wa dunia | Rasilimali ni haba mara kwa mara<br>Uhifadhi wa maji kutishiwa<br>Mafuriko / vitisho vya ukame | Mita za maji, kufuatilia na<br>Kudhibiti uchotaji wa maji<br>Hali ya kuhifadhi maji kwa siku tisini kunahitajika<br>Kudhibiti mafuriko / ukame |

| Kiwango | Hali ya rasilimali | Inavyomaanisha |
|---|---|---|
| Maji chini ya uso wa dunia | Kushuka kwa ubora wa maji au kiwango cha maji | Kubaini na kuweka kwa Gazeti rasmi la Serikali eneo la hifadhi ya maji<br>Mita za maji, kufuatilia na kudhibiti uchotaji wa maji<br>Kuandaa mipango ya usimamizi wa mitiririko maalumu ya maji |
| Ubora wa maji | Mkusanyiko wa maji kupunguza maji sana<br>Uchafuzi wa mazingira kwa kiwango cha juu<br>Hatari kwa maisha ya binadamu iko kwa kiwango cha juu | Kufuatilia na kudhibiti uchafuzi kutokana na maji taka (chanzo cha uchafuzi wa maji taka)<br>Kuanzisha na kushawishi kupunguzwa kwa uchafuzi wowote usiotokana na chanzo cha maji taka |
| Migogoro | Uwezekano wa migogoro upo kwa kiwango cha juu | WRUAs lazima zikuzwe kikamilifu |
| Umiliki wa rasilimali maji | Kutishiwa kwa hali ya juu kwa umiliki wa rasilimali za maji | Kutambua na kuweka kwa gazeti rasmi la Serikali maeneo ya mkusanyiko wa maji yanayotishiwa |
| Kukubalika kwa kwa WRUAs | Kutotambulika kwa kiwango cha juu kwa jukumu la WRUAs na serikali za Kaunti na wadau wengine katika WRM | Kuunganisha shughuli za WRUA SCMPs katika Mipango Jumuishi ya Maendeleo ya Kaunti (County Integrated Development Plans CIDP) |
| **Kiwango 2** | **MAENEO YA TAHADHARI** | |
| Maji juu ya uso wa dunia | Mwenendo unaelekea uhaba wa maji | Kufuatilia na kupanga hatua ya kutenda |
| Maji chini ya uso wa dunia | Mwenendo unaelekea uchotaji mwingi wa maji | Kufuatilia na kupanga hatua ya kutenda |

| **Kiwango** | **Hali ya rasilimali** | **Inavyomaanisha** |
|---|---|---|
| Ubora wa Maji | Mwenendo unaelekea upungufu wa ubora wa maji | Kufuatilia na kupanga hatua ya kutenda |
| Migogoro | Viungo vinavyosababisha migogoro, kwa mfano ukabila, kidini, mgawanyiko wa lugha tofauti | Kuanzishwa WRUAs |
| Umiliki wa rasilimali maji | Rasilimali za maji kuwa katika hali ya kutishiwa | Kutambua na kuweka kwa gazeti rasmi la Serikali maeneo ya mkusanyiko wa maji yanayotishiwa |
| Kukubalika kwa WRUAs | Kutotambulika kwa jukumu la WRUAs na serikali za Kaunti na wadau wengine katika WRM | Kuunganisha shughuli za WRUA SCMPs katika Mipango Jumuishi ya Maendeleo ya Kaunti (County Integrated Development Plans CIDP) |
| **Kiwango 3** | **MAENEO YANAYORIDHISHA** | |
| Maji juu ya uso wa dunia | Rasilimali za maji ni za kutosha kwa wingi kwa ubora wake | Uwezo wa kuhifadhi maji kwa muda wa siku tisini<br>Mita zinahitajika |
| Maji chini ya uso wa dunia | Hakuna madhara yanayodhibitika | Mita zinahitajika |
| Ubora wa Maji | Ubora wa maji wa kutosha, kiwango kidogo cha hatari | Vibali vya uchafuzi kutokana na maji taka zinahitajika |
| Migogoro | Kiwango kidogo cha kutukia hatari ya migogoro | WRUA kuhitajika kwa madhumuni ya ulinzi na uhifadhi wa maji |
| Umiliki wa rasilimali za maji | Rasilimali za maji haziko katika hali ya kutishwa | Kuhifadhi na kulinda rasilimali za maji |

| Kiwango | Hali ya rasilimali | Inavyomaanisha |
|---|---|---|
| Kukubalika kwa WRUAs | Kutambua jukumu la WRUAs na serikali za Kaunti na wadau wengine katika WRM | Kukuza na kuunganisha WRUA SCMPs katika Mipango Jumuishi ya Maendeleo ya Kaunti (County Integrated Development Plans CIDP) |

*Nyongeza C inaonyesha jedwali ambapo chemichemi zote za maji zimegawanywa na kuwekwa katika kundi moja kati ya makundi matatu (Maeneo ya hatari, Maeneo ya tahadhari, Maeneo ya kuridhisha).*

Nia ya WDC ni kutoa kipaumbele kwa mkusanyiko mdogo wa maji katika kiwango HATARI na kiwango TAHADHARI kwa mujibu wa haja ya kutenda kwa haraka. Hata hivyo, inatambulika kwamba mkusanyiko mdogo wa maji katika kiwango cha maeneo yanayoridhisha unaweza kunufaika kwa msaada ili kuzuia hali hiyo kuzorota.

## 2.2 WRUAs Changa

WRUAs changa ni WRUAs ambazo zimeandaliwa na kuhamasishwa kuhusu IWRM na kusajiliwa na msajili wa serikali (AG) na wako tayari kuanzisha SCMP. Hivyo, wanaweza kutafuta msaada wa WDC ingawa maombi yao yatashughulikiwa kama maombi ya kawaida ya WDC.

## 2.3 WRUAs waliokomaa

WRUAs waliokomaa ni WRUAs wale ambao wameanzisha SCMP na wako katika hatua ya utekelezaji. Inatambulika kuwa WRUAs hawa ambao wamefadhiliwa au wameweza kujifadhili na kutoa hesabu kamili ya matumishi ya fedha hizo na kuwa na rekodi nzuri kuhusiana na kufanya shughuli na WRM wanaweza kuidhinishwa kupata ufadhili wa kiwango cha juu. Hata hivyo, wanaweza kufanyiwa uchunguzi wa hali ya juu zaidi, hasa kuhusiana na fedha walizokusanya, na mfumo wa ununuzi na hesabu za matumishi ya fedha. Kiwango cha kanuni kwa kufadhiliwa kwa WRUA iliyokomaa itabidi kuhakikishwa na WRMA.

## 2.4 Shughuli zilizoidhinishwa

Shughuli zilizoidhinishwa kwa kufadhiliwa chini ya WDC ni zile ambazo hukuza malengo. Hizi ni pamoja na:

- Ukusanywaji wa takwimu za msingi: utafiti wa kuchota maji na utafiti wa uchafuzi tafiti za kiuchumi na ustawi wa jamii, na tafiti za rasilimali za maji.
- Kufuatilia matumizi ya rasilimali za maji; kusoma kina cha maji (kiwango cha chemchemi ya maji), Maji chini ya uso wa dunia, Kuangalia Maji juu ya uso wa dunia, Kuangalia vigezo rahisi vya ubora wa maji, kusoma mita kuu za maji;
- Kuandaliwa na kuhamasishwa kwa jamii ili kuunda WRUAs
- Mafunzo / Kujenga Uwezo kwa WRUA na shughuli za kuandaa umma / shughuli za kuhamasisha umma;

- Kupanga miundombinu na maendeleo: mabwawa ya kuhifadhi maji chini ya ardhi, mabwawa ya kuhifadhi maji juu ya ardhi, vidimbwi vya maji, mkusanyiko wa maji kutoka miamba ya kukusanya maji ya mvua, mabwawa ya mchanga ya kuhifadi maji ya mvua katika maeneo kame, kukinga maji kutoka paa za nyumba, matuta yanayojengwa juu ya kilima katika sura ya trapezoid ili kuelekezwa na kukinga maji ya mvua (trapezoid), kuzuia umomonyoko wa ardhi na miundo ya kuhifadhi mikusanyiko ya maji, aina tofauti za kukinga maji (malkas), kuhifadhi maji kwa kina cha mto (river-botom intakes), ulinzi wa kingo za mito - kuta za mwamba zinazojengwa kusaidia uvujaji wa maji polepole zikibakisha unyevunyevu (gabions), miundo ya usafi wa mazingira kwa utoaji wa vifaa na huduma kwa ajili ya utupaji salama wa maji taka (sanitation), miundo ya kupunguza uchafuzi kutokana na maji taka – mabwawa ya kukinga uchafu huu, mashimo ya kutengeza mbolea na miundo mingine ili kupunguza uchafuzi kutokana na maji taka.

- Kuimarisha mifumo ya usimamizi (Rasilimali za watu (HR)), Utumishi, Mawasiliano, Ofisi, usafiri)
- Mafunzo na kuimarisha uwezo wa wadau wa WRUA

- Uhamasishaji wa watumiaji wa rasilimali ya maji na wadau katika shughuli za WRM - ulinzi wa kingo za mito na matumizi bora ya ardhi na kuwakilisha ardhi kwa mchoro, uhifadhi na ulinzi sehemu za ardhi zinazopakana na mito
- Shughuli zinazohusiana na kukabiliana na migogoro ya matumizi ya maji,
- Ujenzi wa maji kwa uchotaji wa maji (Maji juu ya uso wa dunia / Maji chini ya uso wa dunia) (SW / GW) ikiwa ni pamoja na gharama zinazohusiana na mabadiliko ya muundo wa kuhifadhi maji kwa kina cha mto (river-botom intakes), uwekaji wa mita kuu za maji na vifaa kudhibiti uchotaji wa maji
- Uanzishwaji na utekelezaji mipango ya mgao wa maji - Ujenzi na / au uendeshwaji wa shughuli zinazoambatana na uchotaji wa maji au utengano ili kuendana na sheria za WRM

- Uanzishwaji wa vituo vya kupima viwango vya maji na vituo vya kusaidia ufuatiliaji wa wingi na ubora wa hifadhi za maji
- Kulinda mkusanyiko wa maji pamoja na gharama ya miche, mashimo ya kupanda miti, upandaji wa miti, huduma za kutunza na shughuli nyingine
- Shughuli na kazi kwa ajili ya ulinzi wa maeneo ya majimaji, maeneo ya msitu yenye majimaji, na chemichemi nyingine za maji
- Ujenzi wa kudhibiti mtiririko wa maji ambayo hutokea wakati wa mvua nyingi juu ya uso wa dunia, na mmomonyoko wa udongo kama vile mabwawa ya kukinga maji, matuta, sehemu za kukinga maji ya dhoruba na kadhalika
- Ujenzi unaohusiana na ulinzi, uhifadhi au uimarishwaji wa kuboresha rasilimali za maji
- Mapitio ya SCMP
- Kuanzisha utafiti wa mitiririko ya maji na mipango ya usimamizi wa maendeleo ya mitiririko ya maji
- Msaada kwa WRUA juu ya ununuzi na usimamizi wa fedha
- Tathmini ya Athari za Kimazingira na Athari za Kijamii, inapobidi

- Ujenzi unaoambatana na usimamizi wa mafuriko na ukame: hatua za kimuundo na hatua sisizo za miundo kama vile vituo vya uokoaji, vyoo vya juu, Kuimarisha mikakati ya Tahadhari za Mapema, Ramani za Mafuriko Hatari, Vyombo vya kupima viwango vya mvua, kujenga uwezo wa jamii kuhusu usimamizi wa mafuriko, bonde la mto wazi kwa kila mtu, mipango ya usimamizi wa pamoja wa mafuriko, vifaa vya kuhifadhi maji, vifaa vya mgawo wa maji, utaratibu wa kufanya maji yaingie chini ya ardhi

- Msaada wa mapato ya kuishi (Kwa kufadhiliwa mapato ya kuishi tazama mwongozo kuhusu mapato ya kuishi): ufugaji wa nyuki, utengenezaji wa matofali, nyumba ya kijani, ufugaji wa mbuzi, ufugaji wa sungura, ufugaji wa ng'ombe za maziwa, kilimo cha maua, ufugaji wa samaki, ufugaji wa kuku, maendeleo ya bayogesi (biogas), majiko ya kisasa ambayo hutumia ufanisi mafuta machache, lishe la mifugo / uhifadhi wa mbegu wenye kulenga manufaa ya mbegu zisizotumika vizuri (seed banking), kilimo cha alizeti na utoaji wa mafuta yake, Uoshaji wa magari, uwekaji wa maji ya kunywa kwa chupa, vyoo vya kisasa ambavyo hubadilisha choo kuwa mbolea na gesi (Bio-latrines), usimamizi wa taka ngumu, uzalishaji wa zabibu na ufizi, kilimo cha wadudu wanaotengeneza hariri (Silk-worm farming).


- Msaada kwa WRUAs kuhusu ufuatiliaji, usimamizi, uchunguzi ili kuhakikisha kuwa mambo yanaenda sawa, uchunguzi wa ubora au umuhimu na uchunguzi wa ufanisi au manufaa ya miradi inayofadhiliwa.

# 3 UTARATIBU WA UFADHILI WA WDC

## 3.1 Utangulizi

WDC ni mfumo chini ya Mamlaka ya WRMA / WSTF na wadau wengine wa maendeleo ambao hupeana msaada wa kifedha kwa WRUAs zilizoidhinishwa katika shughuli zao za Usimamizi wa Rasilimali za Pamoja za Maji (Integrated Water Resources Management IWRM) kuboresha chemichemi za maji na rasilimali. Utaratibu wa kufadhili kama unavyoonyeshwa kwa Kielelezo 1 unahusisha WRUA kuwasilisha maombi kwa WRMA ambayo baadaye inakaguliwa na halmashauri hiyo ya WRMA. Iwapo maombi yanachunguzwa na kufaulu, basi fedha zinazotolewa kutoka WRMA au WSTF / wadau wengine wa maendeleo. Wakati WRUA imetekeleza shughuli zilizopendekezwa, basi huadaa ripoti ya maendeleo na maombi mapya ya ufadhili. Mzunguko unarudiwa tena.

*Kielelezo cha 1: Utaratibu wa Ufadhili wa WDC*



### 3.2 WRUA Kustahili Msaada wa Kifedha

Kustahili kwa WRUA kuchaguliwa ili kupewa msaada wa fedha kwa WDC kutazingatia kuwa WRUA imetimiza mambo yafuatayo:

1. Cheti cha kusajiliwa kisheria kwa mujibu wa Sheria ya Vyama;
2. Cheti cha kusajiliwa kwa mujibu wa Sehemu ya Pili (Vol 2) Nyongeza K kutoka kwa Mamlaka ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji (Water Resources Management Authority -WRMA)
3. Katiba kama ilivyopitishwa na Mwanasheria Mkuu (AG)
4. Sheria ndogo (Bylaws) za WRUA
5. Kumbukumbu za uchaguzi wa viongozi
6. Akaunti ya Benki na taarifa ya benki;
7. Kumbukumbu za mikutano na Mkutano Mkuu wa kila mwaka (Annual General Meeting AGM);
8. Akaunti zilizokaguliwa na ripoti ya ukaguzi wa fedha kama inahusika
9. Rekodi za Fedha
10. Rekodi za ununuzi (Kotesheni za ununuzi wa bidhaa, ripoti za ufuataji wa thamani za ukaguzi wa uuzaji wa mali kwa zabuni, marisiti, vitabu vinavyowekwa hesabu za fedha, vocha)
11. Kupitishwa na Usimamizi wa chemichemi ndogo za maji (Sub-Catchment Management Plan SCMP)
12. Ripoti za mapato ya kila mwaka kutoka kwa Msajili Vyama
13. Ripoti za maendeleo
14. Muundo wa Usimamizi uliopitishwa kama vile inavyoonyeshwa kwa Sehemu ya Pili: Nyongeza D1
15. Pendekezo la msimamizi wa Uhusiano wa Uuzaji (Supplier Relationship Management SRM) juu ya kukamilika kwa mradi uliofadhiliwa, kama inahusika
16. Regista ya wanachama
17. Kiini cha dhana
18. Mkataba wa Makubaliano na Mamlaka ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji (Water Resources Management Authority -WRMA)

## 3.3 Fomu za maombi / Maombi kwa ajili ya kufadhiliwa

Utaratibu wa maombi utahitaji WRUA kutoa taarifa za msingi kuhusu WRUA, matokeo na shughuli zilizopendekezwa, na bajeti na muda uliopangwa. Utaratibu wa maombi ni sawa na mfumo wa maombi ya msaada wa Fedha. Maombi / ombi ya msaada wa fedha zimetolewa katika Kiambatisho D1 na inatumika hata kama WRUA wanaomba fedha kwa mara ya kwanza au mara nyingine baadaye.

## 3.4 Mpango wa Usimamizi wa Chemichemi ndogo za Maji (Sub-Catchment Management Plan SCMP)

SCMP ni mpango ambao umeanzishwa na WRUA kwa kushirikiana na Mamlaka ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji (Water Resources Management Authority -WRMA) na wadau wengine. SCMP huonyesha seti ya shughuli zilizoundwa ili kufikia malengo yaliyotambuliwa kushughulikia matatizo ya WRM kwenye eneo hilo. SCMP inaweza mara kwa mara kupitiwa upya ili kuhakikisha bado muhimu uliopo kwa masuala ya WRM unajitokeza na kuwa sambamba na mbinu za usimamizi bora. Kwa hivyo, muundo wa SCMP lazima uambatane na ule wa Mkakati wa Usimamizi wa Chemichemi za Maji (Catchment Management Strategies CMS). Muhtasari wa SCMP umetolewa katika Kiambatisho E.

## 3.5 Utaratibu wa Kukaguliwa Maombi

Lengo la WDC la maombi kukaguliwa ni kuchunguza na, kama inahitajika, kuongeza ubora wa maombi. Hii inafanyika kwa njia ya hapo kwa hapo, na ukaguaji wa mashinani. Utaratibu unaweza kurudiwarudiwa WRUA inapoelekea kuboresha vifaa vyake vya maombi ya fedha baada ya kila ukaguzi.

### *3.5.1 Ukaguzi wa hapo kwa hapo*

Mara baada ya kupokea maombi katika Ofisi ya Msajili (the Registrar's Office RO) maombi hukaguliwa hapo kwa hapo na wafanyakazi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji (Water Resources Management Authority -WRMA) wakitumia fomu iliyotolewa katika Nyongeza F. Hatua hii huamua kama maombi yanatimiza mahitaji ya msingi kwa kufadhiliwa na WDC. Maombi

ya hapo kwa hapo lazima kukamilika ndani ya wiki mbili za WRUA kuwasilisha maombi. Ukaguzi huo husaidia kuamua kama faida ya mradi inaambatana na kuhitimu malengo ya WDC. Kwa WRUA kuomba malipo baadaye, lengo la hapo kwa hapo ni kuthibitisha maelezo katika ripoti za kifedha.

#### *3.5.2 Ukaguaji wa mashinani*

Kwa Maombi yanayofaulu ukaguzi wa hapo kwa hapo, hatua ya pili ni ukaguzi wa mashinani. Hii inahusisha ziara za mashinani na wafanyakazi kutoka Ofisi ya Msajili (the Registrar's Office RO) ya Mamlaka ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji (Water Resources Management Authority -WRMA) wakitumia Kiambatisho G. Habari ambayo iko kwa barua ya maombi inakaguliwa kuthibitisha na kuhakikishwa na wanachama wa WRUA, maafisa WRUA na wadau wengine. Kwa WRUA kuomba malipo ya ziada baadaye, lengo la ukaguzi huu ni kuamua thamani ya fedha na kuthibitisha maelezo kwenye ripoti ya fedha yanaambatana na uchunguzi wao wanaoupata mashinani. Uchunguzi huu unapaswa kufanyika katika kipindi cha wiki nne baada ya uchunguzi ule wa kwanza wa hapo kwa hapo. Kulingana na matokeo ya uchunguzi huu wote, maombi ya kufadhiliwa ya WRUA yatapitishwa, kukataliwa au kukubaliwa kuambatana na hali halisi ilivyo.

#### *3.5.3 Shughuli za Makubaliano ya WDC*

Mara baada ya maombi ya mwanzo ya WDC kupitishwa katika uchunguzi wa hapo kwa hapo na pia mashinani, na maombi ya kufadhiliwa ya WRUA yamepitishwa, basi WRUA / Mamlaka ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji (Water Resources Management Authority -WRMA) / Wakfu wa Huduma za Maji (WSTF) na wadau wengine wa maendeleo wataingia kwa mkataba ambao utasimamia utaratibu na masharti yanayohusiana na mgao wa fedha kwa WRUA kwa mujibu wa Nyongeza H.

### 3.6 Utekelezaji wa Usimamizi wa Chemichemi ndogo za maji (Sub-Catchment Management Plan SCMP)

WRUA itatumia fedha zilizotolewa kwa kutekeleza shughuli ilivyoelezwa katika Maombi / Ombi kwa ajili ya kufadhiliwa. WRUA

wanaweza kutafuta msaada wa kitaalamu kutoka kwa Mamlaka ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji (Water Resources Management Authority -WRMA) au kutoka kwa Shirika lolote la Ufadhili (Support Oganisation SO) kama vile ilivyopangwa kuambatana na bajeti.

### 3.7 Ufuatiliaji wa Mamlaka ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji (Water Resources Management Authority -WRMA)

WRMA watakuwa na jukumu la uangalizi katika utekelezaji wa miradi hii. Watakuwa wakifuatilia maendeleo na kutoa msaada wa kitaalamu wakati wa utekelezaji. Matokeo ya ufuatiliaji huu yataorodheshwa na kuwasilishwa ili kuwajulisha WRUA kufikiria masuala ya kufadhiliwa ya siku zijazo.

### 3.8 Ripoti ya Shughuli za Maendeleo

Ripoti ya Shughuli za Maendeleo chini ya WDC inatoa muhtasari wa shughuli zinazofanyika, vikwazo wanavyokabiliwa navyo, masuala yanayojitokeza na matokeo yaliyopatikana. Hii imetolewa kwa mujibu wa Nyongeza I na kuwasilishwa baada ya kila miezi mitatu (au robo mwaka) na mwisho wa kila mzunguko wa ufadhili.

# 4. MWONGOZO WA WDC WA KUFADHILI

## 4.1 Mipaka ya Uwekezaji

WDC ni mfumo ulioundwa ambao mipaka yake ya uwekezaji huimarika wakati nafasi ya uwezo wa WRUA huongezeka. Mipaka ifuatayo hutarajiwa :

1. Shilingi milioni 1.5 kulipwa WRUA kwa jumla mara moja kwa kupokea msaada wa kwanza.
2. Shilingi milioni 5 kulipwa WRUA jumla ya sehemu mbili ambapo wameimarisha mpango Usimamizi wa Chemichemi ndogoza Maji
3. Shilingi milioni 10 kulipwa WRUA kwa kiasi cha mara mbili ambapo wamethibitisha wenyewe kuwa na uwezo wa kushughulikia shilingi milioni 5 ;
4. Kiasi cha juu zaidi cha shilingi milioni 50 kwa WRUA wowote katika kipindi cha mika 10 kwa pamoja;

WRUA wanaweza kufadhiliwa kutoka kwa mashirika mengine ya maendeleo chini ya utaratibu huu lakini mipaka inaweza kutofautiana kuambatana na shirika moja hadi nyingine kulingana na sera za wafadhili wa maendeleo.

## 4.2 Mchango kutoka Mashinani

Mchango kutoka mashinani kwa ajili ya WDC umewekwa kwa kiwango cha chini cha 15% na wanaopata msaada. Mchango wa mashinani unaweza kubadilika kutegemea uwezo uliopo wa WRUA kuongeza mchango wao. Mchango wa mashinani unaweza kuwa kwa njia ya fedha, kazi na vifaa / huduma. Ili kuonyesha thamani ya mchango wa mashinani, miongozo ifuatayo hutumika:

- Kazi ya mkono thamani yake ni KSH 500/- kwa siku kwa wafanyakazi wasio na utaalamu;
- Mchango wa mashinani uwe na thamani ya KSH 300/- . Thamani hii iambatane na WRUA kuchangia muda wao.
- Kazi ya mikono imeidhinishwa tu kwenye shughuli za mradi
- Vifaa na / au huduma thamani yake ni kwa viwango vilivyopo kwenye eneo la WRUA, bei ilivyokubalika na kotesheni tatu za kawaida kwa vifaa vivyo hivyo.

Mchango wa mashinani ni lazima uorodheshwe vizuri na kumbukumbu hizi lazima ziwe zinaweza kupatikana kwa ajili ya ukaguzi.